Haliuzwi
DESEMBA 30, 2025
/islamicftz
Rajab 9 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 564
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah



## Mamlaka zihimiza umakini baada ya mvua kubwa kuacha uharibifu

# Wahadhiri Misk ya Roho walivyoimulika Amani

"Kila mmoja aunde mradi utakaomfaa Akhera"
Sheikh Ally Zuberi, Amiri Basuta



"Amani inapatikana kwa mazungumzo, si vurugu"
Sheikh Abdulkhaliq Issa



"Amani haianzii barabarani bali inaanzia nyumbani"
Sheikh Hassan Abdulshakur



"Mtume, maisha yake, tabia yake na mafundisho yake yalijenga msingi wa Amani ya kweli kwa binadamu wote"
Sheikh Hassan Muhammadayn

"Lengo la kuchagua mada ya Amani ni kutokana na hali ilivyo hivi sasa hapa nchini"
Aref Nahdi, Mwenyekiti The Islamic Foundation

## Rais Erdogan arejea wito kwa Waislamu kushikamana

## Nafasi ya kiapo cha kuitii mamlaka katika kulinda dini na umoja wa kitaifa

NA SHEIKH Shaaban Mussa

## Watanzania tusifanye kosa la Wasudani

Kongamano La 4 La Afrika Mashariki

# TANZANIA

TO OUR SPONSORS,

## Thank You!

PLATINUM SPONSOR

Afya Pure Drinking water

OILCOM

GOLD

ASAS

DAR FRESH

ATN Energies "Excellency in Quality"

AMSONS GROUP

SILVER SPONSOR

USANGU GROUP

AZANIA GROUP

azam MARINE COMPANY LIMITED

azam Pesa

BAKHRESA GROUP

BRONZE SPONSOR

MOROBEST

PBZ IKHLAS PBZ BANK

PEACE Travel & Tours

PGS SECURITY "Leading with tech. Protecting with purpose"

---

Kanzu Point

JAMIIBORA HEALTH SERVICES NETWORK

MEDIA PARTNER'S 2025

azam media

azam tv

2BC2 Wema Unaendelea

DUA tv

AL-HAAJAR TV

tv Imaan Tanzania

Radio Imaan FM

IMAAN NEWSPAPER

IMAAN DIGITAL




Na Yusuph Amin

# Wahadhiri Misk ya Roho walivyoimulika Amani

Historia imeandikwa kupitia mada zilizowasilishwa na Masheikh 'Gen Z' kutoka ndani na nje ya nchi, kwenye Kongamano la nne la Kida'awa la Misk ya Roho Jumamosi ya Desemba 27, 2025.

Katika kongamano hilo lililofanyika kwenye ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam, mada zilizotolewa zimeonekana kuwagusa watu wengi ambapo baadhi yao wamekiri zimewaongezea kiwango cha ufahamu juu ya masuala anuai ya dini na hususan suala la kulinda na kudumisha amani.

Waislamu waliohudhuria walipata ujumbe maridhawa kutoka kwa wahadhiri waliowasilisha mada ambao ni Sheikh Twalib Hassan Ghalib kutoka Uganda, Sheikh Hassan Nsanzimana bin Abdulshakur (Rwanda), na Sheikh Abdulkhaliq Issa Kassim kutoka Kenya.

Wengine ni Sheikh Abdallah Abdulkadir Al–Ahdal na Sheikh Hassan Muhammadayn (wote kutoka Tanzania), na Sheikh Mohammad Imran Asif kutoka Uingereza.

Pia, wanazuoni waandamizi kadhaa walipata fursa ya kuwasalimia Waislamu katika kongamano hilo na kusema machache – wakiwemo Naibu Mufti wa Tanzania, Sheikh Ally Ngeruko, Amir wa Baraza la Sunna Tanzania (BASUTA), Sheikh Ally Zuberi, na Amir wa Baraza Kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislamu Tanzania, Sheikh Mussa Kundecha.

Wengine waliohudhuria ni Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya The Islamic Foundation, Sheikh Ibrahim Twaha na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro (MUM), Sheikh Dkt. Bilal Juma Majuva. Pia, alikuwepo Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt. Ashatu Kijaji na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule.

## Sheikh Hassan Muhammadayn

Mmoja kati ya waliohudhurisha mada na kukonga nyoyo za Waumini ni Sheikh Hassan Muhammadayn, aliyezungumzia nafasi ya Muislamu katika kulinda amani. Katika mada yake hiyo, Sheikh Muhammadayn alisema uwepo wa Mtume ulileta amani kwa majini, wanadamu wa ngazi zote, ndege, wadudu na wanyama.

Akitoa sababu kwanini Mtume Muhammad ni msingi wa amani, Sheikh Muhammadayn alisema maisha yake, tabia yake na mafundisho yake yalijenga msingi wa amani ya kweli kwa binadamu wote. Kupitia tabia yake alifundisha rehma, kupitia uongozi wake alisimamisha haki, na kupitia mafundisho yake alikubali maridhiano badala ya migogoro.

Sheikh Muhammadayn alitaja sababu kadhaa zilizomfanya Mtume kusaini mikataba yenye utata, ukiwamo ule wa Hudaibiya, kuwa ni kuhakikisha amani katika nchi inapatikana.

Alifafanua kuwa, tofauti na viongozi wengi wa leo, Mtume Muhammad alitenda haki na kusimamia ahadi, hata kama wale aliokubaliana nao wanavuka mipaka. Alifanya hivyo kwa sababu Uislamu ni dini ya amani, na si dini ya vita.

Kuhusu maridhiano baina yake na makafiri wa Kikureish, Sheikh Muhammadayn alibainisha kuwa daima Mtume aliishi amani, alifundisha amani na alituachia amani. Alisema, Mtume hakuleta amani kwa nguvu, bali kwa uadilifu, alivumilia kudhuriwa, alisamehe ilihali anao uwezo wa kulipiza kisasi, na alikubali maridhiano badala ya kisasi.

Kuhusu ahadi na uadilifu, alisema Mtume hakuwa na hiyana katika kutekeleza ahadi, hakuwa na hiyana katika kuchunga misingi ya mikataba ya amani aliyoridhia baina yake na maadui zake.

"Hata ukiangalia vita ambavyo Mtume na Masahaba wake walipigana ni kwa sababu walichokozwa, kuonewa au kunyanyaswa. Tukimfuata yeye tunakuwa wajezi wa amani katika familia zetu, jamiii na dunia nzima," aliongeza kusema.

## Sheikh Hassan Twalib Ghalib

Mmoja wa wahadhiri aliyeonekana kuamsha hamasa na kuwagusa watu wengi katika Kongamano la Misk ya Roho, Sheikh Hassan Twalib Ghalib amewataka Waislamu na Watanzania kwa ujumla kulinda amani na kuichunga.

Katika hotuba yake, Sheikh Hassan alitolea mifano nchi mbalimbali ambazo raia wake kwa kushawishiwa walijikuta wakivunja amani katika nchi zao na hivyo kukaribisha matatizo mbalimbali ikiwamo vita vya wenyewe kwa wenyewe vinavyowatesa hadi leo na kujikuta ni wakimbizi katika mataifa mengine.

Sheikh Hassan alisema: "Nchini Libya tulikuwa tukielezwa vijana walipofikia umri wa kuoa waliozeshwa na kupewa mahari na mitaji ya kuanzia maisha, watu kutoka nchi mbalimbali wakiwamo kutoka Afrika Mashariki walienda huko kusoma lakini waliposhawishika wakaingia katika kuvunja amani ya nchi zao, leo wanaishi maisha ya taabu." Aidha, Sheikh Hassan alitolea mfano nchi ya Sudan ambayo wananchi wake baada ya kuandamana na kudai kutomtaka aliyekuwa Rais wao, leo wananchi wa nchi hiyo wamejikuka kwenye mataifa mbalimbali kama wakimbizi, na shughuli nyingine haziendelei kama ilivyokuwa awali.

MEDIA PARTNER'S 2025
azam media · azam tv · 2BC2 Wema Unaoendelea · DUA tv · AL-HAAJAR TV · tvImaan Tanzania · Radio Imaan FM · IMAAN NEWSPAPER · IMAAN DIGITAL

MUHAMMAD صلى الله عليه وسلم "MSINGI WA AMANI"

Na Yusuph Amin

# Amir BASUTA: Kila mmoja aunde mradi utakaomfaa Akhera

Amir wa Baraza Kuu la Jumuiya za Ansaar Sunna Tanzania (BASUTA), Sheikh Ally Zuberi ameitaka jamii ya Kiislamu kuweka mpango (project) sahihi wa maisha yao utakaowawezesha kufanya matendo mema yatakayowawezesha kuingia Peponi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam kwenye kongamano la 4 la Misk ya Roho Jumamosi iliyopita, Sheikh Zuberi alisema ni wajibu wa kila mmoja kuweka mfumo mzuri na sahihi wa maisha ambao una mambo atakayoyafanya na kuwa sababu ya yeye kuipata Pepo ya Allah.

"Kwa sisi Waislamu, kila mmoja ajiulize, je, 'project' yangu katika hii dunia ambayo ni sababu ya kuingia Peponi ni nini?" alisema Sheikh Zuberi na kusisitiza kuwa, uwezo wa mtu na heshima yake ipo katika kile anachokiweza.

Akitolea mfano wa taasisi anayoiongoza (BASUTA), Sheikh Zuberi amesema wanao mradi (project) wa da'awa, ambapo kuna jopo la Masheikh wanaotekeleza jukumu la kulingania Uislamu katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Katika kuhitimisha mazungumzo yake, Sheikh Zuberi alimtaka kila mmoja katika umri wake aangalie ni mradi gani wa amali njema anaweza kuufanya ili umfaae katika maisha yajayo huko Akhera.



MEDIA PARTNER'S 2025
azam media azam tv 2BC2 DUA tv AL-HAAJAR TV tvImaan Tanzania Radio Imaan FM IMAAN NEWSPAPER IMAAN DIGITAL

MUHAMMAD صلى الله عليه وسلم “MSINGI WA AMANI”

Na Yusuph Amin

# Aref Nahdi aonya wanaotumika kuvuruga amani

Mwenyekiti wa taasisi ya The Islamic Foundation (TIF), Aref Nahdi amekemea tabia ya baadhi ya watu wanaojaribu kuvuruga amani, akisema kuwa wengi katika wale wanaotamani Tanzania iingie katika vurugu ni taasisi kubwa duniani iitwayo LGBT.

Nahdi ametoa nasaha hizo katika Kongamano la 4 la Kida'awa La Afrika Mashariki lijulikanalo kama 'Misk ya Roho' lililofanyika Jumamosi iliyopita kwenye ukumbi wa Diamond Jubilee, Jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti Nahdi, taasisi kama LGBT zimekuwa zikijishughulisha na kuhamasisha mambo ya ushoga, mambo mabaya ambayo hayaendani na mila zetu Waislamu na Watanzania kwa ujumla.

Amesema kuwa, Watanzania, hasa vijana ni lazima wafikirie kuwa wanaweza wakatumiwa kwa sababu nyingine za kuleta vurugu lakini wale wanaowahamasisha wanalenga mambo mengine.

“Kwa hiyo tuwe waangalifu sana tunapoletewa hizi fitina. Na tunajua kabisa kuwa walengwa wakubwa ni sisi Waislamu lakini kwa uwezo wa Allah atatulinda, ila na sisi wenyewe tujilinde kuanzia kwenye nyumba zetu,” alisisitiza Nahdi na kusema kuwa maamuzi yao katika jambo lolote yanategemea muongozo wa Allah na Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie).

Nahdi, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kituo cha Masuala ya Ushauri na Huduma za Kifedha za Kiislamu (CIFCA), amesema anatumai 'Generation Z' ya Waislamu imewaelewa na itatumika kuwapa somo 'Generation Z' wengine.



### .... kuhusu Misk ya Roho 2025

Kuhusu kongamano la Misk ya Roho mwaka huu, Nahdi amesema wamechagua mada ya amani kutokana na hali halisi inayoendelea hapa nchini, pamoja na kwamba hivi sasa mambo ni shwari.

“Tunawaomba ndugu zetu Waislamu na wasiokuwa Waislamu kuthamini amani ambayo Allah ametupa, na kutuenzi sisi Watanzania, tusikubali kushawishiwa na tusikubali kuwekewa vitu ambavyo vinatupelekea kuharibu amani ya nchi hii,” alisema.

Aidha, Mwenyekiti Nahdi aliidokeza hadhira iliyokusanyika kwenye kongamano hilo kuwa katika miaka ijayo wamepanga 'Insha Allah' kufanya kongamano la Misk ya Roho jijini Kigali nchini Rwanda.



MEDIA PARTNER'S 2025
azam media azam tv 2BC2 DUA tv AL-HAAJAR TV tvImaan Tanzania Radio Imaan FM IMAAN NEWSPAPER IMAAN DIGITAL

Na Yusuph Amin

# Amir wa Baraza Kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislamu Tanzania aishukuru TIF kwa kurejesha tena kongamano la Misk ya roho

Amir wa Baraza Kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislamu Tanzania, Sheikh Mussa Kundecha ameishukuru taasisi ya The Islamic Foundation kwa kurejesha tena kongamano la Misk ya roho.

Sheikh Kundecha amesema ni jambo jema sana kuwa na kongamano la Misk ya Roho, kwani haliwanufaishi tu watu waliofika ukumbini bali linawanufaisha watu wa ulimwengu mzima, wakiwemo Waislamu na wasiokuwa Waislamu.

"Kikubwa ni kujitambulisha kuwa tupo. Bila kujitambuklisha kuwa tupo, inawezekana tukawa hatupo hata kama 'physically' tunonekana tupo," aliongeza Sheikh Kundecha.

> "Ni jambo jema sana kuwa na kongamano la Misk ya Roho, kwani haliwanufaishi tu watu waliofika ukumbini bali linawanufaisha watu wa ulimwengu mzima
>
> **Sheikh Mussa Kundecha**



MEDIA PARTNER'S 2025

azam media · azam tv · BC2 · DUA tv · AL-HAAJAR TV · tv Imaan Tanzania · Radio Imaan FM · IMAAN NEWSPAPER · IMAAN DIGITAL

# MUHAMMAD صلى الله عليه وسلم "MSINGI WA AMANI"

Na Yusuph Amin



## Sheikh Abdallah Al-Ahdal: Uislamu ulijengwa juu ya amani na mikataba, si mapigano

Sheikh Abdallah AbduLqadir Al-Ahdal amesema Mtume Muhammad alisimamisha misingi ya Uislamu juu ya amani na mikataba, si mapigano.

Akihutubia hadhara ya kongamano la Miski ya Roho, Sheikh Al-Ahdal alisema Uislamu ni dini ya dalili na elimu, na hakuna ruhusa ya kutoa fatwa bila elimu sahihi. Alisisitiza kuwa Sharia ya Kiislamu imekuja kulinda makusudio makuu matano, yakiwemo kuhifadhi dini, nafsi, roho na damu za watu pamoja na mali zao.

Sheikh Al-Ahdaly alisema Uislamu umeweka amani kuwa msingi wa maisha ya mwanadamu, akionya kuwa kuondoka kwa amani ni dalili ya adhabu ya Mwenyezi Mungu. "Kuondoka kwa amani ni dalili ya adhabu ya Mwenyezi Mungu," alisema, akiongeza kuwa Qur'an inawahimiza Waumini kuilinda na kuithamini amani duniani na Akhera.

"Allah huwaadhibu watu kwa hofu na njaa, na akitaka kuwaadhibu zaidi huwaondolea amani," amesema, Sheikh Al-Ahdaly akiongeza kuwa Qur'an inawahimiza waumini kuilinda na kuithamini amani kuanzia duniani hadi Akhera.

Katika kuakisi maisha ya Mtume Muhammad, Sheikh Al-Ahdaly ameieleza hadhara kuwa Mtume aliishi Makka kwa miaka 13 akifundishwa subira, hekima na njia za amani, kabla ya kuhamia Madina ambako aliingia mikataba ya amani na Mayahudi pamoja na wasiokuwa Waislamu kwa lengo la kulinda utulivu wa jamii.

Alitanabahisha kuwa hata wosia wa Mtume katika Hijja ya Kuaga alisema: "Hakika damu zenu ni haramu, mali zenu ni haramu na heshima zenu ni haramu," akibainisha kuwa hakuna ruhusa ya kuvunja heshima, kumwaga damu au kudhulumu mali ya mtu kama msingi wa amani.

Sheikh Al-Ahdaly amesisitiza kuwa amani ni miongoni mwa utajiri mkubwa zaidi wa binadamu, akisema haki ni kuweka kitu mahala pake kwa hekima.

Aliikumbusha hadhara hiyo kuwa kauli kuu ya kongamano hilo akisema, "Mtume Muhammad hakusimamisha dola ya Kiislamu kwa mapigano, bali kwa mikataba na amani," ujumbe uliowagusa wengi na kuakisi kwa kina mada ya kongamano hilo, Mtume: Msingi wa amani.

## Amani ya jamii inaanzia ndani ya familia

Waumini wa dini ya Kiislamu wameambiwa kuwa amani haianzii barabarani bali inaanzia nyumbani.

Kauli hiyo imetolewa na Sheikh Hassan Abdulshakur kutoka Rwanda katika kongamano kubwa la Kiislamu la Miski ya Roho katika hotuba yake nzito iliyojikita katika kuhuisha amani ya kifamilia kama msingi wa amani ya jamii kwa ujumla.

Sheikh Abdulshakur aliwaambia Waumini waliohudhuria kongamano hilo lililoandaliwa na The Islamic Foundation kuwa jamii haiwezi kufikia utulivu wa kweli endapo nyumba hazitakuwa kitovu cha malezi bora, mahusiano yenye haki na amani.

Alibainisha kuwa migogoro ya kijamii, vurugu na mifarakano mingi huota mizizi yake ndani ya familia zinazokosa haki, huruma na mawasiliano sahihi.

Awali, aliusia hadhara kuhakikisha kuwa hao wala haolewi mtu isipokuwa kwa kuzingatia uchamungu (taqwa), akisisitiza kuwa ndani ya uchamungu ndimo zinapopatikana nguzo za amani, mapenzi ya kweli, huruma ya dhati na haki ya kudumu. Alionya kuwa ndoa zisizojengwa juu ya misingi ya kiroho hujikuta zikiyumba pindi changamoto zinapojitokeza, hali inayosababisha migogoro ya kifamilia na kijamii.

Katika hotuba yake, Sheikh Abdulshakur aliwahimiza wanaume na wanawake kutambua na kutimiza haki za kila mmoja kama msingi wa amani ya ndoa.

"Uislamu umeweka mizani ya haki na wajibu kwa pande zote, na ukiukwaji wa haki hizo huondoa sakina (utulivu) na kuacha mianya ya migogoro inayovunja familia na jamii," amesema.

Akirejea maisha ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), Sheikh Abdulshakur aliieleza hadhara namna Mtume alivyokuwa akiishi na wake zake kwa mapenzi, huruma, haki na heshima.

"Mtume hakuwahi kuwa chanzo cha hofu wala dhulma nyumbani, bali alikuwa kimbilio la amani na faraja kwa familia yake," alisisitiza.

Kongamano hilo lilikumbushwa pia namna Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alivyokuwa akiwasiliana na kuamiliana na wake zake kwa hekima, na jinsi walivyokuwa wakishirikiana naye hata katika nyakati za changamoto. Mfano huo umetolewa kama kielelezo cha misingi sahihi ya kujenga familia ya Kiislamu yenye amani na ustawi.

## Sheikh Asif asema elimu ni msingi wa amani

Sheikh Mohammad Imran Asif kutoka Uingereza, amesema elimu ni msingi mkuu wa kujenga amani, maadili na mwelekeo sahihi wa maisha ya Muislamu.

Akizungumza katika Kongamano la Nne la Miski ya Roho linalolenga hadhira ya Afrika Mashariki katika Ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam, Sheikh Imran alisema Uislamu ni dini ya wastani inayojengwa juu ya maarifa sahihi yanayotokana na Qur'an na Sunnah za Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).

"Uislamu ni dini ya wastani (wasatiyyah), unaojengwa juu ya maarifa sahihi yanayotokana na Qur'an na Sunnah za Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani)" alisema Sheikh Imran.

Akifafanua, alisema Sharia ya Kiislamu imekuja kuhifadhi mambo matano dini, maisha, akili, kizazi na mali na kwamba mafundisho ya Mtume Muhammad yamekuwa yakitekelezwa kwa vitendo zaidi ya miaka 1,400 iliyopita, yakilenga kumkomboa binadamu asiwe mtumwa wa mwanadamu mwenzake bali awe mja wa Allah pekee.

Aidha alionya juu ya hatari ya kuifuata dini bila elimu ya kina, akibainisha kuwa "elimu haba ni hatari," kwani huweza kumpeleka mtu katika misimamo mikali au uelewa potofu wa Uislamu.

MEDIA PARTNER'S 2025
azam media azam tv 2BC2 Wema Unaoendelea DUA tv AL-HAAJAR TV tvImaan Tanzania Radio Imaan FM IMAAN NEWSPAPER IMAAN DIGITAL

MUHAMMAD صلى الله عليه وسلم "MSINGI WA AMANI"

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

# Kongole The Islamic Foundation, 'tumestafidi' vya kutosha

Disemba 27, 2025 ilikuwa ni siku ya furaha kwa Waislamu na watu wa imani nyingine pale walipojumuika katika Kongamano kubwa la Misk ya Roho kwa minajili ya kusikiliza ujumbe wa Dini Tukufu ya Uislamu.

Katika kongamano hilo lililofanyika jijini Dar es Salaam, kwenye ukumbi wa Diamond Jubilee, chini ya kaulimbiu "Muhammad – Msingi wa amani", Masheikh watano kutoka ndani na nje ya Tanzania walitoa mada mbalimbali kuhusu amani.

Ni faraja sana kuona tukio la kidini likihudhuriwa na umati mkubwa kama ule, zaidi ya watu 5,000, ndani ya ukumbi wa Diamond Jubilee huku wengine zaidi ya milioni 2 wakifuatilia kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii hapa Tanzania na kwingineko duniani.

Huu ni ushahidi wa athari ya Uislamu, dini pekee ya kweli mbele ya Mwenyezi Mungu. Pia, huu ni ushahidi wa mapenzi ya Waislamu kwa Mola wao na Mtume wao, Muhammad (rehema za Allah na amani imshukie), ambaye moja ya ajenda za msingi alizozinadi kwa walimwengu ni amani.

Katika kongamano lile, Waislamu walipata ujumbe maridhawa kutoka kwa wahadhiri vijana wa ndani na nje ya Tanzania ambao ni Sheikh Twalib Hassan Ghalib kutoka Uganda, Sheikh Hassan Nsanzimana bin Abdulshakur (Rwanda), na Sheikh Abdulkhaliq Issa Kassim kutoka Kenya. Wengine ni Sheikh Abdallah Abdulkadir Al-Ahdal pamoja na Sheikh Hassan Muhammadayn, wote kutoka Tanzania.

Wahadhiri hao waligusia mambo mbalimbali yanayowahusu Waislamu na jamii kwa ujumla. Mambo hayo yameelezwa kwa kina katika habari zilizochapwa katika toleo hili.

Kimsingi, mada zilizowasilishwa katika kongamano la Misk ya Roho 2026 ni muhimu mno, kwani zinahuisha amani na imani, na pia zinatanabaisha juu ya umuhimu wa kushikamana na mafundisho ya Qur'an na Sunna za Mtume (rehema na amani iwe juu yake) katika kila nyanja.

Hivyo, tunasema Waislamu wamevuna elimu kubwa wanayotakiwa kuifanyia kazi ipasavyo kwa ajili ya faida yao ya hapa duniani na kesho Akhera. Tuna kila sababu ya kuwashukuru na kuwapongeza wahadhiri wote, kwani walifanya kazi kubwa ya kukonga nyoyo za wahudhuriaji.

Pia, tunawapongeza watu wote waliohudhuria Kongamano hilo na wale waliofuatilia kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Kuhudhuria kwao ndiyo ilikuwa chachu ya kufanikiwa kwa kongamano hilo, hivyo tunazidi kuwaomba waendelee kushiriki katika makongamano yatakayofuata. Itakuwa ni uchoyo wa fadhila endapo tutahitimisha tahariri hii bila ya kuwapongeza na kuwashukuru wadhamini wote wa Kongamano la Misk ya Roho mwaka huu. Wadhamini hao ni wale wa Platnum ambao ni Afya pure drinking water na Oil com; Dhahabu (Gold sponsors) ni Asas Dairies Ltd ya Iringa, Dar fresh Milk, O-GAS, Amsons Group, na kampuni ya mafuta ya ATN.

Kwa upande wa fedha (Silver) ni Azania Group Companies, Usangu logistics (T) Limited, Azam marine, Azam Pesa na Bakhresa Group. Na shaba (Bronze sponsors) ni MOROBEST, Cargo, Peace Travel & Tours Ltd, PBZ Bank na PGS Security.

Pia, tunawapongeza wadhamini wengine ambao ni Kanzu Point na Jamii Bora kwa kufanikisha kongamano hili adhimu. Tunasema, kazi waliyoifanya wadhamini hawa ni kubwa kwani wamewezesha kongamano kung'ara. Mwisho, tunaupongeza uongozi wa The Islamic Foundation kwa kuandaa kongamano hilo lenye tija, si kwa Waislamu tu bali kwa wanadamu wote.



MEDIA PARTNER'S 2025

azam media · azam tv · 2BC2 · DUA tv · AL-HAAJAR TV · tvImaan Tanzania · Radio Imaan FM · IMAAN NEWSPAPER · IMAAN DIGITAL

MUHAMMAD صلى الله عليه وسلم "MSINGI WA AMANI"



# MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar
0655 763 580

## Misk ya Roho ilivyoimulika Amani













MEDIA PARTNER'S 2025
azam media | azam tv | 2BC2 Wema Unaendelea | DUA tv | AL-HAAJAR TV | tv Imaan Tanzania | Radio Imaan FM | IMAAN NEWSPAPER | IMAAN DIGITAL

MUHAMMAD صلى الله عليه وسلم "MSINGI WA AMANI"




# MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar
0655 763 580

# Misk ya Roho ilivyoimulika Amani




















MEDIA PARTNER'S 2025
azam media | azam tv | BC2 | DUA tv | AL-HAAJAR TV | tv Imaan Tanzania | Radio Imaan FM | IMAAN NEWSPAPER | IMAAN DIGITAL

MUHAMMAD صلى الله عليه وسلم

"MSINGI WA AMANI"

# MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar

0655 763 580

## Misk ya Roho ilivyoimulika Amani















MEDIA PARTNER'S 2025

azam media | azam tv | 2BC2 | DUA tv | AL-HAAJAR TV | tvImaan Tanzania | Radio Imaan FM | IMAAN NEWSPAPER | IMAAN DIGITAL

رَجَب



MAKALA MAALUM

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Nafasi ya kiapo cha kuitii mamlaka katika kulinda dini na umoja wa kitaifa

**Uislamu ni dini inayojenga jamii kwa misingi ya haki, uadilifu na umoja. Miongoni mwa masuala nyeti sana katika Uislamu ni uongozi (imamah), utiifu (twa'ah) na msimamo wa Muislamu katika nyakati za fitna. Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alilizungumzia jambo hili kwa kina, akawaonya Waislamu dhidi ya tamaa ya dunia katika uongozi, na akawaelekeza kuhusu nini cha kufanya wasiporidhika na viongozi wao au pale wanapopotoka.**

**Hadith za Mtume (Allah amshushie rehema na amani) zilizopo katika makala hii zinaweka msingi muhimu wa fikra sahihi za Kiislamu kuhusu siasa, utii wa viongozi na subira.**

## Kiapo cha utii kwa ajili ya ya dunia na adhabu yake

Imepokewa kutoka kwa Abu Huraira (Allah amridhie) kwamba Mtume wa Allah (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Wapo watu watatu ambao Allah hatawaangalia Siku ya Kiyama, hatawatakasa, na watapata adhabu kali mno.

(Wa kwanza ni) mtu aliye na maji ya ziada akamnyima (ile ziada) msafiri (mpita njia). (Wa pili ni) mtu aliyempa kiongozi kiapo cha utii (bay'ah) si kwa ajili ya kitu kingine isipokuwa dunia; akipewa katika hiyo dunia anaridhika, na asipopewa anakasirika. (Wa tatu ni) mtu aliyesimamisha bidhaa yake baada ya Swala ya Alasiri, akasema, 'Naapa kwa Allah ambaye hakuna muabudiwa wa haki isipokuwa Yeye, nilipewa bei fulani na fulani kwa bidhaa hii,' kisha mtu akamsadiki."

Kisha Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akasoma kauli ya Allah: "Hakika wale wanaonunua ahadi ya Allah na viapo vyao kwa thamani ndogo..." [Qur'an 3:77] [Bukhari na Muslim].

Hadith hii inaweka wazi kuwa bay'ah (kiapo cha utii) si biashara, bali ni ahadi ya kidini. Mtu anayemtii kiongozi kwa masharti ya kupata mali, cheo au manufaa fulani binafsi, anapoteza uaminifu wake mbele ya Allah.

Uislamu unataka utiifu uwe kwa ajili ya kusimamisha dini, kulinda umoja wa Waislamu na kuzuia machafuko, si kwa tamaa ya dunia. Hivyo basi, Muislamu anatakiwa awe mkweli katika ahadi zake. Utii unaojengwa juu ya maslahi binafsi huharibu jamii na kuondoa baraka.

## Mabadiliko ya nyakati na kuja kwa viongozi waovu

Imepokewa kutoka kwa Abu Salaam kwamba Hudhaifa bin al-Yamaan (Allah amridhie) amesema alimuuliza Mtume (Allah amshushie rehema na amani): "Ewe Mtume wa Allah, tulikuwa katika hali mbaya, kisha Allah akatuletea kheri, na sasa tupo katika kheri hiyo. Je, baada ya kheri hii kutakuja shari?" Mtume akajibu: "Ndiyo." Hudhaifa akauliza: "Je, baada ya shari hiyo kutakuja kheri?" Mtume akasema: "Ndiyo." Akauliza tena Hudhaifa: "Je, baada ya kheri hiyo kutakuja shari?"Akasema: "Ndiyo." Akauliza Hudhaifa: "Itakuwaje?"

Mtume akasema: "Baada yangu kutakuja viongozi ambao hawataongoza kwa mwongozo wangu, wala hawatafuata Sunna yangu. Na kutatokea miongoni mwao watu wenye nyoyo kama nyoyo za mashetani ndani ya miili ya wanadamu." Hudhaifa akauliza: "Ewe Mtume wa Allah, nitafanyaje nikiyakuta hayo?" Akasema: "Sikia na umtii kiongozi, hata kama mgongo wako utapigwa (kwa uonevu) na mali yako itanyakuliwa (itataifishwa au kuporwa). Sikia na utiii." [Muslim].

Hadith hii inaonesha kwamba kuwepo kwa viongozi madhalimu, madikteta au waliopotoka kimaadili si jambo geni katika historia ya binadamu.

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) hakuwadanganya Swahaba kuwa hali ya haki, uadilifu, amani na utulivu itaendelea milele. Badala yake, aliwaandaa kisaikolojia, kielimu na kiroho kuhusu mtihani na fitna zitakazokuja kwenye zama tofauti, akasisitiza umuhimu wa subira na kulinda umoja wa Waislamu na wa kitaifa.

Funzo kubwa ni kuwa machafuko ya kijamii na umwagaji damu ni hatari zaidi kuliko dhulma binafsi, na subira ina nafasi kubwa katika kulinda jamii. Pia, tunaonywa juu ya uwepo wa viongozi wa upotofu na umuhimu wa kujiepusha na fitna.

Katika riwaya iliyopokewa na Imam Ahmad katika Musnad wake, imekuja kuwa Hudhaifa aliuliza tena: "Kisha nini?" Akajibu Mtume: "Kisha kutakuja waalikaji (wahubiri) wa upotofu. Ikiwa kwenye kipindi hicho utamkuta Khalifa (mteule) wa Allah katika ardhi, basi shikamana naye, hata kama atakuumiza mwili wako na akachukua mali yako. Lakini kama hutamkuta, basi ikimbie fitna kwa kujitenga katika ardhi, hata kama itakubidi ufe hali ukiwa umeshikilia shina la mti."

Riwaya hii inaonesha mizani ya Kiislamu: Uislamu hauamrishi utii wa kibubusa na upofu kwa kila mtu, bali unaelekeza kushikamana na haki, na pale haki inapokosekana, kujiepusha na fitna kunapewa uzito mkubwa.

Si kila anayejiita kiongozi au anayeita watu ni kiongozi wa haki. Elimu na busara ni kinga dhidi ya kupotoshwa. Hivyo basi, kutokana na hadith hizi, Muislamu anapaswa kufahamu kwamba bay'ah (kiapo cha utii) ni ahadi ya kidini, si nyenzo ya maslahi binafsi.

Pili, ni muhimu kufahamu kuwa fitna za uongozi ni sehemu ya mtihani wa umma. Tatu, ifahamike kuwa subira na hekima hulinda jamii zaidi kuliko mihemko. Jambo la nne la kufahamu ni kuwa umoja wa Waislamu ni lengo kubwa la Sharia. Tano, kujiepusha na fitna wakati wa upotofu ni ibada yenye thamani

Nimalize kwa kusema hadith hizi za Mtume (Allah amshushie rehema na amani) zinatoa mwongozo wa kina kuhusu uongozi, utiifu na msimamo wa Muislamu katika nyakati za misukosuko. Zinatuonya dhidi ya tamaa ya dunia, zinatufundisha subira mbele ya dhulma, na zinatuelekeza kwenye kulinda dini na umoja wa Umma.

Muislamu mwenye ufahamu anatambua kwamba maslahi ya dini na jamii yana uzito zaidi kuliko matamanio ya binafsi.

MWANDISHI WETU

# Mamlaka zihimiza umakini baada ya mvua kubwa kuacha uharibifu

**Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mussa Kilakala, alisema wanaendelea kufuatilia na kufanya tathimini ya athari za mvua iliyoambatana na upepo mkali iliyonyesha maeneo mengi wilayani humo usiku wa kuamkia Desemba 28**

Mvua iliyonyesha kwa takribani siku mbili maeneo kadhaa nchini, imesababisha uharibifu wa miundombinu, nyumba kuzingirwa maji na kuathiri safari za treni ya reli ya kisasa (SGR), lakini zikiwa neema kwa baadhi ya sekta.

Desemba 26,2025 Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilitoa angalizo kuhusu uwepo wa vipindi vifupi vya mvua kubwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Singida, Dodoma, Morogoro, Lindi na Mtwara.

Vilevile, Desemba 27 na 28, mamlaka hiyo ilitoa tahadhari kuwa, vipindi vifupi vya mvua kubwa vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Kigoma, Katavi, Tabora, Singida, Dodoma, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Morogoro, Ruvuma, Tanga, Dar es Salaam, Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Lindi na Mtwara pamoja na visiwa vya Pemba na Unguja. Desemba 29, TMA ilitoa angalizo la mvua kubwa kwa maeneo machache ya mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Simiyu, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Morogoro, Ruvuma, Lindi na Mtwara.

## Adha Morogoro

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mussa Kilakala, alisema wanaendelea kufuatilia na kufanya tathimini ya athari za mvua iliyoambatana na upepo mkali iliyonyesha maeneo mengi wilayani humo usiku wa kuamkia Desemba 28.

Alisema hakuna taarifa za madhara ya kibinadamu licha ya nyumba kujaa na kuzingirwa na maji. "Usiku wa kuamkia leo imenyesha mvua kubwa katika maeneo mengi ya Manispaa ya Morogoro, yakiwamo ya kata za Lukobe na Kihonda. Nafuatilia kujua kama kuna madhara ya kibinadamu," amesema.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, Shaban Marugujo, alisema: "Maeneo mengi ya Kihonda na Lukobe yalikuwa yamejaa maji, baadhi ya nyumba zilizingirwa na maji kwa muda mfupi baadaye maji yalipotea. Leo (Desemba 28) kama itanyesha kubwa kama ya jana usiku inaweza kuleta madhara kwa sababu ardhi itakuwa imeshiba maji."

Mariamu Juma, ambaye nyumba yake imezingirwa na maji alisema mvua ilianza saa tisa usiku hadi alfajiri, hivyo maji yalijaa ndani na kuharibu vitu.

Alisema aliokoa watoto wake wawili waliokuwa wamelala chumba cha nje ambacho nacho kilijaa maji. Baada ya mvua kukata anaeleza maji yalipungua.

Aziz Habibu, mkazi wa Kihonda, alisema walilazimika kuwa macho hadi alfajili mvua ilipokatika.



رَجَب

MAKALA MAALUM

Na Said Rajab
0783 650 803

# Mfumo wetu wa elimu una shida gani?

Swali la haraka: Nani alivumbua America? Jibu la uhakika utakalopata: "Christopher Columbus, bila shaka." Tena, mwanafunzi hodari anaweza hata akajua kile kisa mashuhuri kwamba Columbus alidhani amefika India na hivyo kuwaita watu aliyowakuta Wahindi.

Iwapo kutoa maarifa sahihi na kukuza uwezo wa kufikiri kwa kina (critical thinking) ndiyo malengo ya mfumo wa elimu, basi jibu hilo linaonesha kushindwa vibaya kwa mfumo wa elimu ulioenea katika ulimwengu wa Kiislamu leo hii, kwa mambo yote hayo mawili.

Kwa maana, hakuna mwanafunzi anayehoji jambo la wazi kabisa. Mtu anawezaje kupewa sifa ya kugundua ardhi, ambayo tayari ilikuwa inakaliwa na watu wengi? Columbus alikuwa mtu wa kwanza kutoka Ulaya kugundua America, lakini siyo binadamu wa kwanza!

Mamia ya maelfu ya watu wengine (wanaume na wanawake) walifika America kabla yake, na wamekuwa wakiishi pale kwa karne nyingi. Madai kuhusu Columbus yanaonesha wazi 'Euro–centric mindset' (mtazamo wa Kiulaya–ulaya), lakini ajabu upendeleo huu wa wazi unapita bila kutambuliwa wala kuhojiwa!

Huu siyo ukweli pekee wenye mashaka, ambao shule na vyuo vyetu, vitabu, pamoja na walimu wetu wamekuwa wakiutoa. Katika kila nyanja ya masomo wamekuwa wakipitisha mawazo (facts), maadili, dhana, mitazamo, ufafanuzi, fikra, na misingi inayotia shaka ya kisekula, ambayo inapinga Uislamu, huku wenyewe wakiamini kwa dhati kwamba wanatoa huduma ya kukuza elimu.

## Elimu ni jambo bora, lakini tunafundisha nini hasa?

Katika sayansi, tunawafundisha wanafunzi wetu kuutazama ulimwengu kwa mtazamo wa mtu asiyemjua Mwenyezi Mungu. "Na ishara ngapi katika mbingu na ardhi wanazozipitia, lakini bado wanazipuuza." [Qur'an, 12:105].

Utafiti sahihi wa sayansi ungemfanya mtu kufahamu nguvu, ukuu na utukufu wa uumbaji wa Mwenyezi Mungu, unyenyekevu, na vikomo vya maarifa ya binadamu na uwezo wake. Leo hii elimu yetu ya sayansi, ikiwa katika ubora wake, inatoa ujumbe ulio kinyume kabisa. Pia inashindwa kuwawezesha wanafunzi kutenganisha maoni ya wanasayansi kutoka kwenye ukweli wa kisayansi.

Hebu tuulize, katika ulimwengu mpana wa Waislamu, kuna shule yoyote ya Kiislamu inayofundisha sayansi, ambapo wahitimu wake wanaweza kuipa changamoto nadharia ya 'Evolution' ya Darwin kwa misingi ya kisayansi? Tunapofundisha sayansi, je, tunawafundisha watoto wetu kuiweka sayansi mahali pake, kujua upungufu wake? Je, wanaweza kuhoji kwa ustadi muhimu wa kiteknolojia?

Daktari wa tiba hatachukuliwa kuwa ana uwezo iwapo hatajua kasoro za dawa na taratibu za matibabu alizotumia. Mhandisi angechukuliwa kuwa hana sifa iwapo hatajua kasoro ya zana zake. Kwanini basi, ufundishaji wetu wa sayansi haujumuishi mjadala wa upungufu wake?

Kwa sababu, kwa mtazamo wa kisekula, sayansi ndiyo chombo kikuu, ndiyo mwamuzi mkuu wa ukweli na upotofu. Bila hata kutambua, tumekubali pendekezo hilo na elimu yetu ya sayansi inaakisi dhana hiyo. Tatizo halipo kwenye sayansi na teknolojia pekee.

**Hebu tuulize, katika ulimwengu mpana wa Waislamu, kuna shule yoyote ya Kiislamu inayofundisha sayansi, ambapo wahitimu wake wanaweza kuipa changamoto nadharia ya 'Evolution' ya Darwin kwa misingi ya kisayansi?**

Wasomi wetu bora kabisa wa Shahada za Uzamili katika Usimamizi wa Biashara (MBAs), wamejifunza kuwa lengo la biashara ni kuongeza faida (maximise profits), lengo la kufanya masoko (marketing) ni kuunda mahitaji (create demand), na njia sahihi ya kufanya uamuzi wa kibiashara ni kupitia uchanganuzi wa faida na gharama (cost benefit analysis).


Yote hayo yana msimamo thabiti machoni pao, na yanaleta mashaka katika uhalisia, kama yalivyo madai kuhusu Christopher Columbus. Wahitimu wetu bora kabisa wa Uandishi wa Habari (Journalism) hawana mfumo tofauti wa uandishi wa habari na ule uliosisiwa na watu wa Magharibi.

Hawana 'definition' yao wenyewe ya habari, kusudi lao la kukusanya habari, au viwango vyao wenyewe vya kimaadili, ambavyo lazima viratibu usambazaji wake. Katika somo la uchumi tunafundisha kwamba wanadamu ni wanyama wanaoongeza mahitaji (utility–maximizing animals), wakitawaliwa na mpangilio wa mahitaji wa Maslow (Maslow's hierarchy of needs).

Katika ufundishaji wetu wa historia, tunaona matukio yanayotokea bila ya kuwepo hesabu ya kimaadili inayoendesha matukio hayo. Katika masomo ya Saikolojia au Sosholojia, Tiba au Uhandisi, Civics au Jiografia, habari ni hiyo hiyo.

Kiukweli, shule na vyuo vyetu vimekuwa vyombo vikuu vya kueneza usekula katika jamii za Waislamu. Zimekuwa zikifundisha kwa ufanisi kwamba, Uislamu hauna uhusiano wowote na kuuelewa ulimwengu huu au katika kutatua matatizo yake.

***Itaendelea wiki ijayo Insha Allah***



MWANDISHI WETU

# Mwinyi: Ujenzi wa shule za ghorofa suluhisho la uhaba wa madarasa

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali itaendelea kutekeleza mkakati wa ujenzi wa skuli za ghorofa kama suluhisho la kudumu la changamoto ya uhaba wa madarasa na uendeshaji wa skuli kwa mfumo wa zamu ya asubuhi na mchana.




Rais Dkt. Mwinyi ameyasema hayo alipoifungua Skuli Mpya ya Msingi ya Muungano iliyopo Kibanda Maiti, Mkoa wa Mjini Magharibi, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ameeleza kuwa Serikali inalenga kuongeza bajeti ya sekta ya elimu hadi kufikia Shilingi Trilioni Moja na kuifanya sekta hiyo kuwa sekta mama ya kipaumbele kwa maendeleo ya nchi.

Rais Dkt. Mwinyi amesema tayari Serikali imeshasaini mkataba na Benki ya CRDB wenye thamani ya Shilingi Bilioni 240 kwa ajili ya ujenzi wa skuli 29 za ghorofa, ambapo maandalizi ya ujenzi yameanza katika maeneo ya Fuoni Kibondeni, Jumbi na Chunga kwa Unguja, pamoja na Kiuyu Minungwini, Mchanga Mdogo na Micheweni kwa Pemba kupitia mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Rais Dkt. Mwinyi amebainisha kuwa Serikali ya Awamu ya Nane tayari imejenga skuli 35 za ghorofa, hali iliyosaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani, ingawa bado yapo maeneo yenye changamoto hiyo hususan Mkoa wa Mjini Magharibi unaobeba zaidi ya nusu ya wakazi wa Zanzibar.



Rais Dkt. Mwinyi amesema uimarishaji wa miundombinu ya elimu si suala la hiari bali ni wajibu wa Serikali ili kuhakikisha kila mtoto anapata mazingira bora ya kujifunzia, sambamba na kulinda misingi ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 ya haki, usawa na upatikanaji wa huduma za msingi ikiwemo elimu.

Katika kuimarisha rasilimali watu, Rais Dkt. Mwinyi amesema Serikali imeajiri walimu wapya 1,741 katika mwaka 2024/2025, na tayari imeajiri walimu 492 katika mwaka wa fedha 2025/2026, huku lengo likiwa ni kuajiri walimu 1,500 pamoja na kuboresha maslahi yao.

MWANDISHI WETU



# Mwinyi auzindua mji wa Dkt. Hussein Mwinyi

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe.Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ameuzindua rasmi Mji wa Dkt. Hussein Mwinyi uliopo Mombasa, Mkoa wa Mjini Magharibi, na kuutaka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kuendelea kujikita katika utekelezaji wa miradi mikubwa yenye tija kwa maendeleo ya Taifa.

Rais Dkt. Mwinyi ameyasema hayo wakati wa uzinduzi wa mji huo wa kisasa, tukio lililofanyika ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Amesema mifuko ya hifadhi ya jamii imekuwa chachu ya maendeleo katika nchi nyingi duniani, na kuipongeza ZSSF kwa kuanza vema utekelezaji wa mradi huo mkubwa wa maendeleo, hususan katika ujenzi wa makazi ya kisasa na ya gharama nafuu.

Aidha, Rais Dkt. Mwinyi ameishauri ZSSF kujikita zaidi katika uwekezaji wa miradi mikubwa ikiwemo miradi ya nishati ya umeme, baada ya kufanya vizuri katika ujenzi wa masoko, vituo vya mabasi na nyumba za makaazi.

Rais Dkt. Mwinyi ameeleza kuwa wakati umefika kwa Zanzibar kuwa na miji mipya ya kisasa yenye haiba na ubora, ili wananchi waishi katika makaazi bora na mazingira salama. Ameongeza kuwa bado wananchi wengi wanaishi katika makaazi duni na mitaa isiyopimwa, hali inayosababisha changamoto za kimazingira na kupanga miji, na hivyo kuwataka wananchi kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuleta maendeleo.

Halikadhalika, uzinduzi wa Mji huo umeenda sambamba na uzinduzi wa nyumba za gharama nafuu pamoja na uzinduzi wa msikiti mpya uliojengwa katika eneo hilo, Masjid Balad Salaam.

> “Wakati umefika kwa Zanzibar kuwa na miji mipya ya kisasa yenye haiba na ubora, ili wananchi waishi katika makaazi bora na mazingira salama
>
> **Rais Dkt. Hussein Mwinyi**

Rais Dkt. Mwinyi amewataka ZSSF na wakaazi wa Mji wa Dkt. Hussein Mwinyi kuzitunza nyumba hizo kwa kushirikiana, ili ziendelee kuwa na haiba na ubora kwa muda mrefu.

Vilevile, Rais Dkt. Mwinyi ameridhia ombi la ZSSF la kupatiwa eneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi katika Mji wa Serikali Kisakasaka, na kuiagiza Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuipatia taasisi hiyo eneo la ardhi kwa ajili ya ujenzi huo, huku akisisitiza kuwa ofisi zitakazojengwa ziwe bora na za mfano.




# OIC kujenga Uganda chuo kikuu cha uuguzi kwa wanawake Afrika

Shirika la Ushirikiano wa Kiislamu (Organisation of Islamic Cooperation – OIC) limetangaza mpango wa kuhamasisha nchi zake wanachama 57 kufadhili ujenzi wa chuo kikuu cha kwanza barani Afrika cha uuguzi kwa wanawake, kitakachojengwa chini ya Islamic University in Uganda (IUIU) limeripoti gazeti la Monitore la Uganda.

Akizungumza wakati wa kukabidhi jengo jipya la madarasa katika shule ya uuguzi ya wanawake katika kampasi ya Kabojja, Nateete, jijini Kampala, Katibu Mkuu Msaidizi wa OIC anayesimamia sayansi na teknolojia, Aftab Ahmad Khokher, alisema mradi huo ni mfano halisi wa mafanikio yanayopatikana pale nchi za Kiislamu zinapounganisha nguvu kufadhili elimu.

"Kampasi hii inaakisi juhudi za pamoja za OIC katika kuiwezesha jamii ya Waislamu kupata elimu, kwa sababu elimu ndiyo moyo wa jamii, na mwanamke aliyeelimika ndiye msingi wa familia zetu leo," alisema Khokher.

Aliongeza kuwa chuo hicho kitatoa mchango mkubwa si Uganda pekee bali pia kwa nchi jirani na dunia kwa ujumla, hasa katika kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya wauguzi waliobobea.

Kwa upande wake, Mkuu wa IUIU, Ismail Ssimbwa Gyagenda, alisema chuo hicho kiko katika hatua ya kuimarisha miundombinu na rasilimali watu. Alibainisha kuwa idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka 8,000 hadi 14,500, na matarajio ni kwamba idadi ya wanafunzi wa uuguzi itaongezeka zaidi kadri maprofesa wanavyoongezeka.

Mradi huu unatazamwa kama hatua muhimu katika kuimarisha elimu ya afya kwa wanawake na kukuza maendeleo ya kijamii barani Afrika.







# Mufti Uganda ataka ushirikiano mpana wa Waislamu Afrika

Mufti wa Uganda, Sheikh Shaban Ramadhan Mubaje, amekutana na viongozi wa Jumuiya ya Waislamu kutoka Burkina Faso na kutoa wito wa kuimarishwa kwa ushirikiano wa Waislamu barani Afrika kupitia elimu, ujenzi wa taasisi imara na mazungumzo ya dini mbalimbali.

Kikao hicho kilifanyika katika makao makuu ya Baraza Kuu la Waislamu la Uganda (UMSC) jijini Kampala.

Mufti Mubaje akimkaribisha Rais wa Jumuiya ya Waislamu wa Burkina Faso, Al Hajj Moussa Koanda, alisema mkutano huo unalenga kuimarisha mahusiano kati ya jumuiya za Waislamu wa Afrika Magharibi na Mashariki. Katika mazungumzo hayo, elimu na maendeleo ya taasisi yalitambuliwa kuwa nguzo muhimu za ushirikiano wa bara zima.

Akizungumza baada ya mkutano huo, Al Hajj Koanda aliipongeza UMSC ambayo iliazishwa 1972 kwa kiwango chake cha juu cha mpangilio na uongozi, akisema uzoefu wa Uganda ni mfano unaoweza kuigwa na nchi nyingine za Afrika.



Alisisitiza kuwa Waislamu wa Afrika wanapaswa kujipanga vyema na kufanya kazi kwa karibu ili kukabiliana na changamoto zinazofanana.

## Cameroon yazindua mpango kuhamasisha fedha za Kiislamu

**Cameroon, wiki hii,m imezindua kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha sekta ya huduma ya fedha za Kiislamu jijini Yaoundé, tovuti ya businessincameroon inaripoti. Hafla hiyo iliyoongozwa na Wizara ya Fedha ya Cameroon iliwakutanisha wadau wakuu wa sekta ya fedha lengo ikiwa ni kukuza ujumuishaji wa kifedha kwa kuingiza uchumi usio rasmi—ambao unahusisha idadi kubwa ya wananchi—katika mfumo rasmi wa benki.**

**Kwa sasa, utekelezaji unafanyika kupitia mfumo wa madirisha ya Kiislamu (Islamic windows), ambapo benki za kawaida zimeidhinishwa kutoa huduma za kifedha zinazoendana na Sharia.**

**Serikali pia imetenga takribani faranga bilioni 3 za CFA hadi mwaka 2027 kama dhamana ya awali ya kuimarisha sekta hiyo, hatua ambayo wachambuzi wanaitaja kama maandalizi ya muda mrefu ya kuanzisha soko la hati fungani za Kiislamu (Sukuk) kufadhili miradi mikubwa ya miundombinu, kuepuka gharama kubwa za masoko ya kawaida ya madeni.**

## Pakistan yajizatiti kupambana na riba

**Katika mkakati wa kufuta mfumo wa riba nchini Pakistan, benki za Kiislamu zimeambiwa zithibitishe kuwa ni za Kiislamu kwa vitendo na mwenendo wa kifedha.**

**Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Pakistan (SBP), Saleem Ullah, akizungumza katika hafla moja ya mahafali, amesema benki za Kiislamu zinawakilisha mfumo wa fedha ulio wazi na wa kimaadili, uliowekwa mfano wake zaidi ya miaka 1,400 iliyopita kupitia biashara za Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).**

**Alizitaka benki na wataalamu wa fedha za Kiislamu kuwa mfano bora kwa kuzingatia maadili na kuhakikisha wateja wanaelewa kikamilifu kuwa miamala yao iko huru na masharti ya siri au riba iliyojificha. Kwa upande wake, Rais na Mkurugenzi Mtendaji wa Sindh Bank, Muhammad Anwar, alisema benki za Kiislamu ni bora zaidi kuliko benki za kawaida. Alitangaza kuwa matawi 60 kati ya 330 ya benki hiyo yatabadilishwa kuwa ya Kiislamu mwaka 2025, mengine 150 mwaka 2026, na yaliyosalia 120 kukamilisha mabadiliko hayo mwaka 2027.**

MAKALA MAALUM

Na Said Rajab
0783 650 803

# Watanzania tusifanye kosa la Wasudani

**Katika miezi ya karibuni, kabla ya kufanyika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, niliandika makala katika gazeti hili nikitahadharisha kwamba kuna watu waovu wanatamani kuleta vurugu za kisiasa na kuondoa amani ya nchi yetu.**



# Watanzania tusifanye kosa la Wasudani

Katika miezi ya karibuni, kabla ya kufanyika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, niliandika makala katika gazeti hili nikitahadharisha kwamba kuna watu waovu wanatamani kuleta vurugu za kisiasa na kuondoa amani ya nchi yetu.

Mwanasiasa mmoja alizungumzia suala la 'kukinukisha' na 'kufanya uasi', Maaskofu wa kanisa lake wakaja juu na kuitisha Serikali, eti imuachie mara moja, tena bila masharti yoyote! Wakati kesi yake ilipoanza kusikilizwa, tuliona watu kutoka Kenya, wengine wakilazimisha kuingia nchini mwetu bila hata kufuata taratibu za uhamiaji wakitaka kuja Mahakamani kusikiliza kesi hiyo iliyotangazwa mno na vyombo vya habari vya Magharibi.

Mabalozi wa nchi za Ulaya pamoja na wanaoitwa 'Wanaharakati' wa haki za binadamu walijaa mahakamani kufuatilia mwenendo wa kesi hiyo ya uhaini. Mara tukaona maazimio ya Bunge la Ulaya yakiishinikiza Serikali ya Tanzania kumuachia huru mwanasiasa huyo wa upinzani, kama yalivyokuwa matamko ya Baraza la Maaskofu la Kanisa Katoliki Tanzania (TEC).

Ilipofika siku ya Uchaguzi Mkuu, Oktoba 29, 2025 ndipo Watanzania walipoona tafsiri halisi ya 'kukinukisha' na 'kufanya uasi', kama ilivyokusudiwa na mwanasiasa huyu na wachochezi wenzake wa vurugu zile zilizopangwa, ambazo ziliitwa maandamano ya kudai haki!

Zipo nyakati ambazo ukiwa nacho kitu hujui thamani yake, lakini kikipotea ndipo unajua thamani yake. Ndugu zangu Watanzania, tuitunze na kuidumisha amani yetu kwa gharama yoyote ile, na tuwapuuze watu waovu wanaoeneza fitina, chuki na uchochezi unaolenga kuvuruga amani ya nchi yetu kupitia mitandao ya kijamii.

Walibya walijazwa upepo na wale walioitwa 'Wanaharakati wa kudai haki' wakamuondoa Kanali Muammar Gaddafi madarakani, hivi sasa wanajuta. Zile 'haki za binadamu na demokrasia' walizoahidiwa mpaka wakaamua kuivuruga nchi yao nzuri, hawajawahi kuiona, wachilia mbali kuipata! Hayo ndiyo matokeo ya akili za kushikiwa!

Kule Sudan, wakati wa utawala wa Jenerali Omar Al–Bashir, aliibuka binti mmoja mdogo wa miaka 22, mwanafunzi wa Chuo Kikuu, ambaye alipambwa kwa sifa nzito za 'mpigania haki wa Sudan' dhidi ya utawala ulioitwa wa kidikteta wa Omar Al–Bashir.

Binti huyu (Alaa Salah) ambaye unaweza kumuita Mange Kimambi wa Sudan, aliwachochea wananchi wa Sudan kufanya uasi dhidi ya Serikali ya Jenerali Omar Al–Bashir kupitia maandamano mfululizo yaliyochukua miezi kadhaa akisaidiwa kwa kiasi kikubwa na mataifa ya Magharibi.

Kutokana na kutojitambua kwa wananchi wengi wa Sudan, wakamkabidhi Alaa Salah akili zao na maisha yao wakidai anapigania haki zao na kuwakomboa kutoka kwa yule waliyemuita 'Dikteta' Omar Al–Bashir. Wakanasa kwenye mtego wa mabeberu wa Magharibi kupitia uchochezi wa binti huyu!

Vyombo vya habari vya Magharibi vilimpaisha sana binti huyu na vikampa jina la 'Mwanamapinduzi mwanamke wa Kisudani.' Alivishwa kilemba cha ukoka na mabeberu wa Magharibi kwa kuweza kuwahamasisha Wasudani kwa namna ya kipekee nchi nzima kuipinga Serikali yao.

Mwezi Desemba 2018, Serikali ya Sudan chini ya Jenerali Omar Al–Bashir ilijaribu kunusuru anguko la kiuchumi lililosababishwa na miaka mingi ya vikwazo vya Marekani, ambavyo vilileta hasara kubwa kwenye mapato ya sekta ya mafuta kwa kuchukua hatua ngumu za dharura ikiwemo kushusha thamani ya sarafu yake.

Serikali iliondoa ruzuku kwenye mkate na mafuta, jambo ambalo liliwapa kisingizio watu wabaya kuanzisha maandamano Mashariki mwa nchi hiyo wakipinga hali ngumu ya maisha na kusababisha hasira iliyosambaa mpaka mji mkuu, Khartoum. April 11, 2019, Al–Bashir aling'olewa madarakani kupitia mapinduzi ya kijeshi, nchi ikaongozwa na Baraza la Mpito la Kijeshi.

Kwa sababu malengo ya mapinduzi yale hayakuwa kuwakomboa Wasudani, ambao walitumika tu kufanikisha ajenda za mabeberu wa Magharibi, jeshi la mapinduzi likagawanyika vipande viwili. Hivi sasa Sudan haikaliki tena na wananchi wake wanateseka kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Maelfu wameuawa na wengine wapo kwenye kambi za wakimbizi. Huyu Alaa Salah, mwanamke aliyekuwa nembo ya kile kilichoitwa 'mapinduzi' nchini Sudan, ambayo yalipigiwa debe sana na vyombo vya habari vya Magharibi, sasa anaishi maisha mazuri jijini London, Uingereza, wakati watu wake wanaogelea kwenye mabwawa ya damu, wakiteseka kutokana na matokeo ya vitendo vyake.

Kosa walilofanya Wasudani la kushikiwa akili na mwanaharakati Alaa Salah, ndilo hilo hilo wanalifanya baadhi ya Watanzania kwa kushikiwa akili na wanaharakati kama Mange Kimambi, Maria Sarungi na genge lao.

Huyu, Alaa Salah, kwa msaada mkubwa wa vyombo vya habari vya Magharibi na mitandao ya kijamii alifanikiwa kumfitinisha aliyekuwa Rais wa Sudan Jenerali Omar Al–Bashir na wananchi wake mpaka akaondolewa madarakani kupitia maandamano yasiyo na kikomo.

Kilichojaa kwenye akili za Wasudani wakati ule ni "Al–Bashir anakula neema za nchi peke yake na familia yake." Hawakufikiria familia zao zitakuwaje baada ya hapo, wazazi wao wanaowategemea kiuchumi watakuwaje, mali zao walizozitafuta kwa muda mrefu zitakuwaje.

Wakaingia barabarani na kuharibu nchi yao walioijenga wenyewe kwa jasho na damu, kwa sababu tu ya chuki waliyopandikizwa dhidi ya Rais Al–Bashir, na kisingizio walichopata cha kupanda kwa bei ya mkate.

Sasa ni mwaka wa saba tangu kufanyika kwa mapinduzi ya kijeshi yaliyomuondoa madarakani Jenerali Omar Al–Bashir nchini Sudan. Mwanamke yule aliyesifiwa sana haonekani tena kwenye vyombo vya habari vya wale walimsifu! Wasudani waliokuwa naye bega kwa bega wengi wao wako makaburini, na wengine ni vilema wa kudumu.



Mtindo huo huo ndiyo unatumika hivi sasa kumchafua Rais Samia na familia yake kwa lengo la kumfitinisha na wananchi wa Tanzania ili waandamane kumpinga. Mara kauza bandari kwa Waarabu, mara anauza mashirika ya umma, mara anahamisha mali za Watanganyika kwenda Zanzibar, na porojo nyingine nyingi kama hizo! Ni propaganda tu zenye dhamira mbaya!

Watanzania tuzinduke, kuna watu waovu wanapanga na kuratibu vurugu zinazolenga kuiangusha dola kwa kuwatumia wananchi wasiojitambua. Mara nyingi Qur'an huwazindua watu wanaofanya mambo bila ya kuangalia matokeo yake kwa kuwaambia: "Hivi nyie hamna akili?", "Je, hamzingatii?", "Je, hamtafakari?

# رَجَب فتاوى



**SHEIKH**
**Shaaban Mussa**
**0786 272 323**

**Swali: Je, Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa mwanasiasa?**

**Jibu:** Iwapo aliyelouliza swali anakusudia neno siasa kwa maana ya kuwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa na sifa za uongozi, uwezo wa kuwaongoza watu, na kusimamia mambo yao kwa namna inayowaletea maslahi yao, basi hilo ni kweli. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa mwanasiasa.

Hata hivyo, neno siasa katika Uislamu halimaanishi ujanja, hila au udanganyifu, bali linamaanisha kusimamia mambo ya watu kwa haki na kwa kuzingatia maslahi yao (siyāsah shar'iyyah). Kwa maana hii, Mtume wa Allah (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa kiongozi na mwanasiasa wa kiwango cha juu kabisa.

Sababu zinazothibitisha hilo ni kwamba aliunganisha dini na uongozi wa jamii, aliongoza kwa haki, hekima na huruma, aliweza kusimamia masuala ya amani, vita, mikataba na mahusiano ya kijamii, na aliongoza kwa lengo la kheri ya dunia na Akhera.

Kwa hiyo, siasa yake ilikuwa sehemu ya Utume wake, si siasa zisizo na haki wala zisizo na maadili.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alimkusanyia sifa hizi kwa ukamilifu uliowazidi wanasiasa na viongozi wote waliomtangulia na waliomfuata, hadi siku ambayo Mwenyezi Mungu atairithi ardhi na vilivyomo juu yake.

Yeyote anayechunguza maisha ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) kabla ya Utume na baada yake, katika nyakati za amani na vita, na katika mahusiano yake na marafiki pamoja na maadui, ataona mambo ya ajabu mno. Haya yote ni kwa sababu Mwenyezi Mungu alimchagua kwa Utume na akamteua kwa Risala, ili awaongoze watu wote na kuiongoza jamii ya binadamu kuelekea kheri ya dunia na Akhera.

Kwa hakika, Manabii waliomtangulia walikuwa wakiiongoza kila mmoja kaumu yake pekee, kama ilivyokuja katika Hadith sahihi katika Bukhari na Muslim, na lafudhi ni ya Muslim, kutoka kwa Abu Huraira (Allah amridhie) aliyesema:

"Wana wa Israil walikuwa wakiongozwa na Manabii; kila alipofariki Nabii alifuatwa na Nabii mwingine, na hakika hakuna Nabii baada yangu."

Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu alimpa Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) upekee wa kutumwa kwa watu wote, akamjaalia uongozi wa wanadamu wote, na akamfanya kuwa mfano wa kuigwa na kila mmoja. Kupitia kwake, aliwatoa watu kutoka gizani kwenda kwenye nuru, na akawakusanya baada ya kutawanyika.

Hata maadui na wapinzani wake walimshuhudia kuwa alikuwa na siasa njema na mipango mizuri. Na kweli ni ile inayoshuhudiwa hata na maadui. Hakika, kila anayemuiga na kujifunza kutoka katika siasa na uongozi wake huwa karibu zaidi na mafanikio.

Kwa hiyo, yeyote anayejishughulisha na siasa za kuwaongoza watu anapaswa kumuiga Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), ajifunze wasifu wake (Sira), na ajifunze kutokana na siasa na uongozi wake. Hakika Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ni mwalimu bora kabisa kwa kila anayelitaka jambo jema.

Kuthibitisha hilo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Kwa hakika kabisa mna mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anayemtarajia Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho."

(Qur'an, 33:21)

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali: Siku za hivi karibuni kulikuwa na vurugu katika mji wetu zilizoambatana na uharibifu wa taasisi na mali za makampuni mbalimbali. Watu walichoma moto na walichukua mali zilizokuwamo. Nami pia, kwa kufuata mkumbo, nilishiriki na nikachukua baadhi ya vitu. Baada ya kushikamana na dini nimetambua kuwa jambo hilo haliruhusiwi. Nifanye nini kuhusu vitu hivyo?**

**Jibu:** Ni wajibu wako kama Muislamu kurudisha vitu hivyo kwa wahusika wake, kwani ulivichukua bila haki. Haijuzu kuvimiliki wala kunufaika navyo.

Iwapo unawajua wamiliki wake, ni lazima uvirejeshe kwao. Na ikiwa huwajui wamiliki wake au huwezi kuwafikia, basi unapaswa kuviwasilisha kwa mamlaka husika kama serikali za mitaa au vyombo vya usalama, au kuviacha katika eneo salama kwa namna inayowezesha wahusika kuvipata.

Pia, ni wajibu wako kutubia toba ya kweli, kuacha kabisa kurudia kitendo hicho, na kumrejea Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa unyenyekevu. Jishughulishe na utiifu Wake, ongeza ibada za sunna, na zidisha istighfari. Huenda Mwenyezi Mungu akakusamehe, akaipokea toba yako, na akakuhitimishia kwa matendo mema.

Aidha, tunakushauri wewe na Waislamu wote—wanaume na wanawake—kujisitiri na fujo zinazokiuka mali, roho na heshima za watu, kwani hazina uhusiano wowote na maadili ya Uislamu.

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali: Je, kauli hii ni sahihi? Kwamba sisi kama Waislamu hairuhusiwi kabisa kutumia istilahi ya uhuru, hata kama kinachokusudiwa ni uhuru unaojengwa juu ya itikadi ya Kiislamu?**

**Jibu:** Kwa hakika, neno uhuru linaweza kutumika likikusudiwa uhuru wa kibinadamu unaohifadhi heshima ya mtu, unalinda utu wake, na kuhifadhi haki na mali zake.

Uislamu umeupa uhuru wa aina hii umuhimu mkubwa, umeweka misingi na kanuni zake, na ulikuwa mtangulizi katika hilo kwa maneno na kwa

MAHMOUD NYAMGUMA

# Rais Erdogan arejea wito kwa Waislamu kushikamana



Rais wa Uturuki Recep Tayyip Erdoğan amewataka Waislamu duniani kushikamana na kuepuka mifarakano kwani wao ndio waathirika wakuu wa misukosuko mikubwa ya kiusalama na kibinadamu inayoikabili dunia akitoa mifano ya Palestina, Lebanon, Sudan hadi Syria.

Akizungumza katika mkutano wa Umoja wa Wanademokrasia wa Kimataifa (UID) uliofanyika katika Ikulu ya Rais, Erdoğan amesema mshikamano wa Kiislamu ni ngao muhimu dhidi ya dhuluma, migogoro na wasiwasi unaotikisa Ulaya na Asia.

Akieleza hali ya Palestina, Erdoğan amelaani mashambulizi ya Israel aliyoyataja kuwa ni ya kikatili yaliyoharibu makazi ya zaidi ya Wapalestina milioni 2.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la kuratibu masuala ya kibinadamu OCHA (OCHA), zaidi ya asilimia 70 ya miundombinu ya makazi Gaza imeathiriwa tangu kuongezeka kwa mashambulizi, huku maelfu ya raia wakiuawa au kujeruhiwa.

Nchini Lebanon, mashambulizi ya mpakani yamesababisha maelfu ya watu kuyahama makazi yao, hali inayoongeza mgogoro wa kibinadamu katika eneo lenye mvutano wa muda mrefu.

Rais huyo pia ameizungumzia Syria, akisema wananchi wake wanaendelea kupambana kujijenga upya baada ya zaidi ya miaka 14 ya vita. Takwimu za Benki ya Dunia zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 90 ya Wasyria wanaishi chini ya mstari wa umaskini, hali inayotokana na vita, vikwazo na hujuma za ndani na nje.

Erdoğan amesisitiza kuwa ni wajibu wa umma kusimama pamoja katika kusaidia waliodhulumiwa na kulinda utu wa mwanadamu.

Katika hotuba hiyo, Erdoğan amelitaja pia jukumu la diaspora ya Kituruki barani Ulaya kama nguzo muhimu ya nguvu ya umma. Alisema licha ya kukumbana na ubaguzi wa rangi, chuki na mashambulizi ya kigaidi, hasa Ujerumani ambako kuna zaidi ya Waturuki milioni 3, diaspora imeendelea kushikamana na imani, utambulisho na mchango wao kwa Uturuki na nchi wanazoishi. Kulingana na takwimu za Eurostat, jamii za wahamiaji Waislamu zimechangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa Ulaya kupitia ajira, kodi na ujasiriamali.

Erdoğan aliwakosoa vikali wanasiasa wa upinzani wanaodharau diaspora na Waislamu kwa ujumla, akisema kauli hizo zinachochea chuki na kudhoofisha mshikamano wa kitaifa, na kusisitiza kuwa Waislamu popote

## Shujaa wa Australia aliyebadili mitazamo hasi dhidi ya Waislamu

**Tukio la ushujaa lililofanywa na Ahmed Al-Ahmed katika mashambulizi huko fukwe za Bondi mjini Sydney, limeweka wazi namna simulizi potofu kuhusu Waislamu zinavyoshindwa kabisa zinapokutana na uhalisia wa maisha.**

**Kwa muda mrefu, Waislamu wamekuwa wakiwasilishwa kwa taswira ya vurugu, chuki na kutojali uhai wa wengine.**

**Hata hivyo, katika tukio hilo, bila kauli, bila propaganda na bila maandalizi, Muislamu mmoja alisimama kulinda uhai wa binadamu wenzake, akionesha kwa vitendo kuwa simulizi hizo hazina mizizi katika ukweli.**

**Ushujaa wa Ahmed Al-Ahmed haukuwa ajali wala tukio la kipekee lisilo na msingi. limetokana na maadili ya Uislamu yanayojengwa juu ya utu, heshima na kulinda uhai wa mwanadamu.**

**Qur'an inaweka wazi kuwa kuokoa uhai wa mtu mmoja ni sawa na kuokoa uhai wa watu wote, msimamo unaojenga dhamira ya kumlinda binadamu bila ubaguzi. Katika dakika za hatari, thamani hii haikubaki kwenye maandiko, bali iligeuka kuwa kitendo halisi cha kujitolea.**

**Kwa mujibu wa Sunna, Muislamu wa kweli hupimwa kwa matendo yake kwa watu wengine, usalama wake, maneno yake na vitendo vyake. Ahmed Al-Ahmed amethibitisha hilo kwa kusimama mbele ya hatari, akitanguliza uhai wa wengine kuliko wake mwenyewe.**

**Kitendo cha Ahmed kilivunja hoja dhaifu inayodai kuwa Uislamu unafundisha chuki au ukatili, na badala yake kikadhihirisha kuwa Uislamu ni dini ya rehema, ujasiri na uwajibikaji wa kijamii.**

**Simulizi potofu huishi kwa sababu ya ujinga na upotoshaji, lakini huporomoka zinapokutana na mifano hai ya maadili yanayotekelezwa. Ushujaa wa Ahmed Al-Ahmed umeonyesha kuwa Uislamu hauhitaji kutetewa kwa maneno mengi bali kwa**




MAKALA MAALUM

Na Wwandishi wetu

# Vyombo vya ulinzi, siasa na kauli za viongozi wastaafu

Katika mijadala ya kisiasa katika mfumo wa vyama vingi, kumekuwa na kauli nzito zinazotolewa na baadhi ya watu waliowahi kushika madaraka nyeti ya uongozi wa nchi.

Kauli mojawapo inayozua maswali makubwa ni pale mtu wa aina hiyo — ambaye kwa uzoefu na elimu yake hawezi kuitwa mjinga — anapotumia vyombo vya habari kudai kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vimegawanyika na vimeanza kujihusisha na michakato ya siasa. Kauli ya aina hii haiwezi kupuuzwa kirahisi, kwani hubeba ujumbe mzito kwa wananchi, kwa dola, na kwa mustakabali wa utulivu wa nchi.

Swali la msingi ni: mtu wa aina hii huwa anamaanisha nini hasa, au anataka kuwaaminisha wananchi nini? Je, ni kweli anazungumza kwa kutokujua anachokifanya, au ana mkakati na ajenda za siri za kisiasa alizozificha kwenye pazia la lugha za onyo na tahadhari?

Kwanza, ni muhimu kukumbuka kuwa kwa mtu aliyewahi kuwa sehemu ya uongozi wa juu wa nchi, hasa wakati wa mfumo wa chama kimoja, ana ufahamu mpana wa namna dola inavyofanya kazi. Anaelewa majukumu ya vyombo vya ulinzi na usalama, mipaka yao, na uhusiano wao na mamlaka ya kisiasa.

Katika mfumo wa chama kimoja, vyombo hivyo vilikuwa karibu zaidi na dola tawala kwa sababu dola na chama vilikuwa karibu kuwa kitu kimoja. Hivyo, mtu huyo anajua vizuri kuwa hata katika mfumo wa vyama vingi, vyombo vya ulinzi haviwezi kuacha kuwa na uhusiano wowote na siasa, kwa maana ya ulinzi wa nchi, wananchi, Katiba, amani, na mchakato wa kidemokrasia.

Kwa hiyo, anapodai hadharani bila takwimu kuwa vyombo vya ulinzi "vimegawanyika" au "vinafanya siasa," kuna uwezekano mkubwa kuwa analenga kuunda taswira fulani kwa wananchi, aghlabu kuashiria kuwa nchi au mchakato fulani wa kisiasa hauko salama, kwamba kuna upendeleo, au kwamba dola haitakuwa mwamuzi wa haki wakati wa marekebisho ya Katiba au uchaguzi. Huu ni ujumbe unaoweza kuwafanya wananchi waogope, wakose imani na taasisi za dola, au waamini kuwa matokeo ya uchaguzi tayari yamepangwa.

Pili, kauli kama hizi mara nyingi hutumika kama mtaji na kinga ya kisiasa. Mtu au kundi linalohisi linaweza kukosa fursa au kushindwa katika ushindani wa kisiasa hutafuta sababu za mapema za kuelezea kushindwa huko.

Badala ya kukiri udhaifu wa sera, ujumbe au uungwaji mkono wa wananchi, lawama huhamishiwa kwa vyombo vya ulinzi na usalama. Kwa kufanya hivyo, wanajenga hoja ya kuwa "uwanja haukuwa sawa," hata kabla ya uchaguzi kufanyika.

Tatu, ni vigumu kuamini kuwa mtu huyo hajui majukumu ya vyombo vya ulinzi kabla, wakati na baada ya uchaguzi. Kabla ya uchaguzi, vyombo hivi vina wajibu wa kuhakikisha usalama wa mikutano ya kisiasa, wagombea na wananchi kwa ujumla. Wakati wa uchaguzi, vina wajibu wa kulinda vituo vya kupigia kura, vifaa vya uchaguzi na amani ya wapiga kura bila kuingilia maamuzi ya kisiasa. Baada ya uchaguzi, vina jukumu la kudhibiti vurugu zozote, kulinda mali na watu, na kuhakikisha kuwa nchi inaendelea kuwa na utulivu. Haya yote ni majukumu ya kikatiba, si "kufanya siasa."

Kwa hiyo, kudai kuwa utekelezaji wa majukumu haya ni "kujihusisha na siasa" ni kupotosha maana halisi ya kazi za vyombo vya ulinzi na usalama. Kauli kama hizi zinaweza kuwa hatari kwa sababu zinavuruga imani ya wananchi kwa taasisi ambazo ndizo nguzo ya amani ya taifa.

Historia ya nchi nyingi inaonesha kuwa pale imani kwa vyombo vya ulinzi inapodhoofishwa kwa makusudi, migogoro ya kisiasa huwa rahisi kugeuka kuwa migogoro ya kijamii au hata ya kijeshi.

Mwisho, ni wajibu wa wananchi kusoma kauli hizi kwa macho ya tahadhari. Si kila kauli inayotolewa na mtu aliyewahi kuwa kiongozi mkubwa ni ya kweli au inalenga maslahi ya taifa. Wakati mwingine ni sauti ya maslahi binafsi au ya kisiasa yanayojificha nyuma ya hofu ya umma.

Vyombo vya ulinzi na usalama vinapaswa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Katiba na sheria, huku vikiepuka vishawishi vya kisiasa. Wanasiasa nao wanapaswa kuwajibika kwa maneno yao, kwa sababu kauli zao zinaweza kujenga au kubomoa misingi ya amani na umoja wa kitaifa.

Afya
Pure Drinking water

"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.

WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com



رَجَب

MAKALA MAALUM



NA SHEIKH SEIF RUGA
0712 690 811

# Sharia ya wosia na hukumu zake katika Uislamu

**Sharia ya Kiislamu imejipambanua kwa kutimiza maslahi ya watu na kuwafanya waishi kwa furaha. Sharia hii imekuja kurahisisha na kuondoa uzito katika maisha ya waja, kwa kuzingatia mahitaji yao na hali zao.**

**Miongoni mwa mifano ya urahisishaji huu ni kuwekwa sharia ya wosia kupitia Kitabu cha Allah na Sunna za Mtume (rehema na amani ziwe juu yake). Wosia ni njia ya kuondoa matatizo na kuwanufaisha masikini kwa kutoa sehemu ya mali kwa hiari. Muumini huonesha shukrani kwa Allah kwa neema hiyo aliyopewa, na huifanya mali yake kuwa na sehemu ya haki kwa wenye uhitaji. Allah anasema: "Na katika mali yao ipo haki ya mwenye kuomba na asiyeomba." [Qur'an, 51:19].**

**Kadhalika, Mtume wa Allah amesema "Siyo haki Muislamu mwenye kitu cha kuusia akalala (nacho) usiku miwili bila wosia wake kuandikwa karibu yake." [Bukhari na Muslim]. Hadith hii inasisitiza kuharakisha kuandika wosia ili kuhakikisha haki na wajibu unatekelezwa.**

**Wanazuoni wa sharia ya Kiislamu wametoa maana mbalimbali za wosia. Miongoni mwa maana hizo ni: "Wosia ni umiliki unaohusishwa na muda baada ya kifo (cha aliyeusia) kwa njia ya kujitolea (sadaka) – iwe ni mali au manufaa yake."**

**Wosia umethibiti katika Qur'an, pale Allah Mtukufu aliposema: "Mwenyezi Mungu anakuusieni juu ya watoto wenu..." [Qur'an, 4:11]. Miongoni mwa hekima ya kuwekwa sharia ya wosia ni kuwawezesha watu kufanya matendo mema wanapotoa msaada wa kheri, kuimarisha undugu na uhusiano kwa jamaa wasiorithi, kusaidia wenye shida na kuziba mahitaji ya maisha yao.**

## AINA TANO ZA WOSIA

### Mosi, wosia wa wajibu

Huu ni wosia kwa mwenye deni, au mwenye kuhifadhi amana za watu, au mwenye jukumu la faradhi alilopaswa kutekeleza, kama vile utoaji wa zaka, utekelezaji wa ibada ya Hijja, n.k.

### Pili, wosia wa sunna

Huu ni wosia kwa jamaa wasiorithi, mashirika ya kheri, na wenye uhitaji. Wanazuoni wa madhehebu ya Hanbali wamesema, ni sunna kwa aliye na mali nyingi kuacha wosia. Hii ndiyo kauli mashuhuri kwa madhehebu yao. Imeelezwa kwamba, inapendeza kwa tajiri kuusia thuluthi moja ya mali yake, na kwa mwenye mali ya wastani kuusia sehemu ya tano (1/5) ya mali yake.

### Tatu, wosia wa mubaha (si wajibu wala sunna)

Mfano wake ni wosia kwa matajiri miongoni mwa ndugu au jamaa wengine. Wanazuoni wa madhehebu ya Hanbali wamesema, ikiwa mtu hana warithi, basi inaruhusiwa kuusia mali yake yote; na hii ndiyo rai ya wanazuoni wao wengi.

### Nne, wosia unaochukiza (makruhu)

Baadhi ya wanazuoni wamesema, inachukiza kuacha wosia kwa mtu asiye na mali nyingi. Kadhalika, inachukiza ikiwa mwenye kuusia ni masikini, au warithi wake wana uhitaji mkubwa wa mali hiyo. Lakini ikiwa warithi si wahitaji, basi haichukizi.

### Tano, wosia wa haramu

Mfano wake ni wosia wa maasi na mambo yaliyoharamishwa, kama vile kuusia kujenga nyumba ya kutenda maovu, au kwa ajili ya sherehe za maasi na matambiko ya kishirikina.

## NGUZO NNE ZA WOSIA

Kwa mujibu wa Jopo la Wanazuoni wa Kiislamu (Jumhur Al–Ulamaa), wosia una nguzo kuu nne zifuatazo:

### Kwanza, mwenye kuusia

Huyu ni mtu anayemilikisha kitu (mali) chake kwa mtu mwingine kwa ridhaa yake, lakini mali au kitu hicho kitatumika baada ya kifo chake. Ni sharti kwa anayeusia awe amebaleghe na mwenye akili timamu.

Aidha, mwenye kuusia awe mmiliki wa mali anayoiusia na asiwe na deni linalomeza mali yake yote, pia awe radhi kwa hiari yake kwa sababu kuusia ni kitendo cha kumilikisha. Kwa hiyo, haikubaliki wosia wa mtu anayetania, aliyelazimishwa au aliyekosea, kwa kuwa mambo haya yanaondoa ridhaa.

### Pili, mwenye kuusiwa

Huyu ni mtu anayepokea umiliki wa kitu kilichousiwa baada ya kifo cha mwenye kuusia, na anaweza kuwa mtu binafsi au taasisi, ambapo umiliki wa kitu cha wosia huhamishiwa kwake baada ya kifo cha mwenye kuusia.

Mwenye kuusiwa – iwe taasisi au mtu binafsi ni sharti awe na uwezo wa kumiliki mali wakati wa kifo cha mwenye kuusia. Na wosia hauwezi kufanywa kwa mtu aliyekwishafariki.

### Tatu, kitu kilichowekwa wosia

Hii ni mali au haki (manufaa) inayohusiana na wosia, ambayo humilikishwa kwa njia ya wosia. Umiliki wa mali au haki hiyo hutekelezwa baada ya kifo cha mwenye kuusia, alimradi kitu au mali hiyo iliyowekewa wosia haitokani na chumo la haramu au kuendeleza maasi.

Mfano wake ni kama kuusia kujenga kumbi au nyumba zinazochochoea mambo machafu na maovu, uharibifu wa maadili, na kueneza ufisadi katika jamii. Huu ni wosia batili kwa makubaliano ya wanazuoni.

### Nne, maneno ya wosia

Hili ni tamko au kauli rasmi ya kuusia inayojumuisha tamko la kutoa usia (Al–ijabu) na kukubali (Al–qabul). Tamko la usia hutimia kwa kila neno linaloonesha kutoa mali baada ya kifo, kama vile: "Nimekuusia hiki", au "Mpeni fulani kiasi hiki baada ya kifo changu", au maneno mengine yenye maana sawa na hayo. Wosia, pia hutimia kwa maandishi, kama ilivyo kwa maneno, kwa mujibu wa makubaliano ya wanazuoni.




# Uchamungu ni vazi linalohitaji kulindwa

**Taqwa, au uchamumgu ni vazi analotakiwa avae kila Muislamu. Kutokana na umuhimu wake, Muislamu anahimizwa kujipamba kwa vazi hili ili kutimiza lengo la kuumbwa. Mwenyezi Mungu anatuambia: "Enyi wanadamu! Kwa hakika tumekuteremshieni nguo za kuficha tupu zenu, na nguo za pambo. Na nguo za uchamungu ndiyo bora..." [Qur'an, 7:26].**



Pia, kumcha Allah ni dalili ya imani, na ni sababu ya mja kuweza kudumu katika njia iliyonyooka (iliyo sawa). Ni kwa sababu hiyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehema na amani imfikie) mara kwa mara alikuwa akiwausia na kuwakumbusha Masahaba juu ya Taqwa.

Ni vizuri ieleweke wazi hapa kuwa, uchamungu si kuikimbia jamii, au kuyakimbia matatizo yaliyomo ndani yake na kwenda kuishi porini, bali ni mtu kuishi ndani ya jamii huku akijiepusha na matatizo ya kimaadili yaliyomo ndani ya jamii hiyo.

Muhimu kuliko yote ni Muislamu kujibidiisha na kumcha Allah katika vipengele vyote vya maisha. Qur'an Tukufu na Sunna za Mtume, kwa pamoja vinasisitiza hilo ili Muislamu aweze kudumu na utekelezaji wa amali anazoziridhia Allah.

Iwapo mtu atakwenda kinyume na lengo hili (uchamungu), anatahadharishwa na adhabu ya duniani na kesho Akhera. Ukweli ni kuwa, mja anaposhindwa kumcha Allah huwa mbali na uongofu, kama anavyobainisha Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Je, tuwafanye walioamini na wakatenda mema kama wafanyao uharibifu katika nchi? Au tuwafanye wachamungu kama waovu?" [Qur'an, 38:28].

Jambo moja la faida ni kwamba, moyo wa Muislamu kamwe hauwi mzuri isipokuwa kwa taqwa. Ili kufikia lengo ni muhimu kushikamana na msingi mkuu wa taqwa ambao ni kufuata Qur'an na Sunna za Mtume (rehema na amani iwe juu yake). Kwa kufuata viwili hivi ndipo tutafikia daraja ya uchamungu na hivyo kupata uongofu na amani ya Allah hapa duniani na kesho Akhera.

## Uchamungu ni mahala popote na wakati wote

Katika hali ya kawaida, mafanikio ya mwanadamu huanza kuonekana wakati anapoanza kuchukua hatua za kidogo kidogo. Hivyo kila anayehitaji kupata mafanikio ni vizuri akajilazimisha kumcha Mola wake. Allah anatujuza: "Basi mcheni Allah kadiri muwezavyo (mwisho wa jitihada yenu)..." [Qur'an, 64:16].

Jambo muhimu la kuzingatia ni kuishi kwa kumuogopa Allah wakati wote na mahala popote. Si maana ya uchamungu kumuogopa Allah mbele za watu na kumuasi faraghani. Kinachotakiwa kwa Muislamu ni kutekeleza maamrisho ya Allah na Mtume kivitendo na kuepuka makatazo pamoja na mambo mengine yenye utata (shubuhaat).

Katika kusisitiza hilo, Mtume (rehema na amani ya Allah imfikie) amesema: "Mche Allah popote ulipo, na fuatisha kitendo kiovu kwa kitendo kizuri ili kifute (kitendo kibaya), na ishi na watu kwa tabia nzuri." [Sahih Tirmidhi].

## Matunda ya uchamungu

Allah Ta'ala ameufanya uchamungu kuwa zawadi bora yenye kumfaa mwanadamu Siku ya Kiyama, kama anavyosisitiza: "... na jitengezeeni zawadi. Na kwa hakika bora ya zawadi ni uchamungu. Na nicheni Mimi, enyi wenye akili." [Qur'an, 2:197]. Kwa munasaba wa kauli hii ya Allah, ni wazi hatuwezi kuwa Waislamu wa kweli ikiwa nyoyo zetu hazijajisalimisha na kukubali kumcha yeye.

Hii inatokana na ukweli kuwa, uchamungu si msingi tu wa Uislamu, bali pia ni sharti la imani ya kweli. Miongoni mwa matunda ya uchamungu ni haya yafuatayo. Mosi ni kumtoa mwanadamu katika hali zote za utumwa (ibada) wa viumbe na kumbakisha katika utii wa amri za Mola wake na kuepuka makatazo.

Zaidi ni kwamba, mtu mwenye sifa ya uchamungu kamwe hasumbuliwi na mambo yenye kuangamiza watu, ambayo moja ya sababu zake ni kuitii nafsi kwa kufuata inachotaka. Pia, uchamungu ni njia ya uongofu ambayo mja akishikamana nayo humsaidia kuelekea kwa Mola wake bila ya kuwa na hofu ya malipo.

Qur'an yatuambia: "Hakika wachamngu wanastahiki kufuzu (Siku ya Kiyama)." [Qur'an, 78:31]. Na kutoka kwa Abu Huraira (Allah amuwie radhi) amesema, Mtume (rehema na amani ya Allah iwe juu yake) aliulizwa, "Ni kitu gani kitakachowaingiza watu kwa wingi Peponi?" Akasema: "Kumcha Mwenyezi Mungu na tabia njema." [Tirmidhi].

Ama faida nyingine ni mja kuruzukiwa kwa urahisi. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu ambaye anasema: "...na anayemcha Mwenyezi Mungu humtengenezea njia ya kutokea. Na humruzuku kwa njia asiyotazamia..." [Qur'an, 65:2–3]. Allah azithibitishe nyoyo zetu katika dini, vilevile awaongoze Waislamu wenzetu ambao kwa namna moja au nyingine wameghafilika na kuifuata dini.




SEHEMU YA 3

MUSSA IMANI
SHEHA,
ZANZIBAR
0773 181 494



# USAMA BIN ZAID

## Kipenzi cha Mtume na mtoto wa kipenzi cha Mtume

## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Ushindi wa Usama dhidi ya Warumi: Katika toleo lililopita tuliona jinsi Khalifa Abubakr alivyoamuru jeshi lililoandaliwa na Mtume (Allah amshushie rehema na amani) kabla ya kufariki kwake liendelee chini ya uongozi wa kijana shujaa, Usama bin Zaid bin Haritha (Allah awaridhie).**

**Usama aliendа na jeshi hilo lililojumuisha Maswahaba wakubwa wakubwa mpaka wakafika miji ya Al-Balqaa na Qal'at Daaroum upande wa Palestina, kama alivyoelekezwa na Mtume (Allah amshudhie rehema na amani) bila matatizo yoyote.**

**Waislamu walipokutana na maadui wao, Usama alionesha umahiri mkubwa wa kijeshi, na baada ya mapambano makali, Waislamu waliwashinda vibaya maadui wao.**

### Athari yake

Ushindi wa Usama uliacha athari kubwa na muhimu katika harakati za kuueneza Uislamu katika maeneo hayo kwani uliiondoa hofu ya kuwaogopa Warumi katika nyoyo za Waislamu, na kuifungua njia ya kuishinda miji yote ya Sham, Misr na kaskazini mwa Afrika.

Kisha Usama alirudi na jeshi lake akiwa amempanda farasi wa baba yake, akibeba ngawira nyingi kutoka kwa Warumi. Inasemekana kuwa hakuna jeshi lililorudi kutoka vitani likiwa salama na lenye ngawira nyingi kuliko jeshi la Usama. [Taz. Suwarun min Hayat As-Sahaba, uk. 231].

### Maisha ya Usama baada ya Mtume

Baada ya kufariki kwa Mtume, Usama alibaki na imani madhubuti, ucha-Mungu, ushujaa pamoja na tabia zote njema. Aliheshimiwa na akaheshimika, na kupendwa sana na Waislamu.

Inasemekana kuwa katika utawala Umar (Allah amridhie) Khalifa huyo alimuwekea Usama fungu (mafao) makubwa zaidi kuliko mafao ya mwanawe Abdallah. Abdallah akamwambia: "Baba, unampa Usama dirham elfu nne na mimi unanipa elfu tatu, ilhali baba yake hakuwa na ubora (nafasi) katika dini kuliko ulionao wewe, na wala Usama hana ubora nilionao mimi?"

Umar akamjibu: "Hapana. Baba yake alipendwa zaidi na Mtume kuliko baba yako, naye (Usama) alipendwa zaidi na Mtume kuliko wewe." Baada ya maelezo hayo, Abdallah aliridhia mgao aliopatiwa na baba yake.

### Tujifunzayo

Kuna mengi ya kujifunza katika historia ya Swahaba Usama. Miongoni mwa hayo ni kwamba heshima na unyenyekevu ni misingi muhimu ya kuijenga jamii bora.

Tazama Abubakr, Umar pamoja na wakuu wenzao walivyojishusha mbele ya Usama, lakini pia tazama heshima ya Usama mbele ya Makhalifa hao. Waislamu tujipambe na tabia hizi kwani kinyume chake ni kiburi na kujiona.

Kiongozi katika nafasi yoyote anapaswa kujua vipaji vya anaowaongoza ili avitumie kwa maendeleo ya Umma wa Waislamu. Mtume alimfuatilia Usama, akagundua kipawa chake cha uongozi na ushujaa, na akamchagua kuliongoza jeshi licha ya udogo wake wa umri.

Allah awe radhi na Usama pamoja na Maswahaba wote. Wabillahi tawfiq.




AFYA YAKO

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Sekta ya afya Gaza inahitaji msaada mkubwa, haraka

**Mgogoro wa kiafya unaoikumba Gaza umefikia kiwango cha kutisha, huku wataalamu wa afya wakionya kuwa athari zake hazitaisha leo wala kesho, bali zitaathiri vizazi kadhaa vijavyo. Kwa mujibu wa makala ya kitabibu iliyoandikwa na Dkt Robert Glatter, daktari wa afya ya umma anayechangia katika jarida la kimataifa la uchambuzi Forbes, Gaza kwa sasa imegeuka kuwa "jangwa la huduma za afya" kutokana na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya kitabibu.**

## Mfumo wa afya uliokuwa dhaifu hata kabla ya vita

Hata kabla ya Oktoba 7, 2023, Ukanda wa Gaza ulikuwa na hospitali 36 pekee—idadi ambayo ilishindwa kukidhi mahitaji ya zaidi ya watu milioni mbili. Dkt Glatter anaeleza kuwa mfumo wa afya Gaza ulikuwa tayari dhaifu kutokana na mzingiro wa muda mrefu wa Israel na Misri tangu mwaka 2007, uliosababisha uhaba wa dawa, vifaa tiba, umeme na mafuta. Wagonjwa waliokuwa na magonjwa sugu kama saratani, figo, moyo na mfumo wa fahamu walilazimika kusaka matibabu nje ya Gaza.

Katika mazingira hayo, baadhi ya hospitali za Israel zilikuwa zikitoa huduma maalumu kwa wagonjwa wa Kipalestina kupitia mpango wa kibinadamu uliogharimiwa na Mamlaka ya Palestina. Ushirikiano huo pia ulihusisha mafunzo ya kitabibu na tafiti za pamoja kati ya wataalamu wa Israel na Palestina—mipango ambayo ilisimama kabisa baada ya vita kuanza.

## Hospitali zimeharibiwa, huduma zimesambaratika

Kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa (UN) zilizonukuliwa katika makala ya Forbes, kufikia Oktoba 21, 2025, ni hospitali 14 pekee kati ya 36 za Gaza zilizokuwa zikifanya kazi, tena kwa kiwango cha chini. Zaidi ya asilimia 94 ya hospitali zote zimeharibiwa au kuangamizwa.

Hali hii imesababisha hospitali zilizosalia kulemewa kupita uwezo wake, huku zikikabiliwa na mazingira yasiyo salama kiafya, uhaba wa maji safi, chakula na malazi. Upungufu huu umechangia kuenea kwa magonjwa miongoni mwa wagonjwa na wahudumu wa afya wenyewe.

## Njaa na utapiamlo: tishio linaloendelea

Ripoti ya Desemba 19, 2025 ya Integrated Food Security Phase Classification (IPC), ilionya kuwa licha ya kusitishwa kwa mapigano kupunguza kasi ya baa la njaa, hali bado ni tete sana. Ripoti hiyo, iliyoandaliwa kwa kushirikiana na World Health Organization, UNICEF, World Food Programme na Food and Agriculture Organization, inaeleza kuwa watu zaidi ya milioni 1.6—sawa na asilimia 77 ya wakazi wa Gaza—wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa chakula.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, zaidi ya watoto 100,000 pamoja na wanawake 37,000 wajawazito au wanaonyonyesha wanatarajiwa kukumbwa na utapiamlo mkali hadi Aprili 2026 iwapo msaada wa chakula na huduma za afya hautaongezwa kwa kiwango kikubwa na endelevu.

## Wahudumu wa afya: waliuawa, waliokimbia, waliokosekana

Mgogoro huu pia umeathiri vibaya nguvu kazi ya sekta ya afya. Shirika la Medical Aid for Palestinians, kama linavyonukuliwa na Forbes, linaripoti kuwa zaidi ya wahudumu wa afya 1,722 waliuawa kati ya Oktoba 2023 na Septemba 2025—wastani wa zaidi ya wahudumu wawili kwa siku.

Wengine wengi wamelazimika kukimbia Gaza, huku baadhi wakizuiliwa kwa nyakati tofauti, hali iliyosababisha upungufu mkubwa wa wataalamu wa afya.

## Elimu ya afya yasambaratika kabisa

Athari za vita zimeifikia pia sekta ya elimu. Dkt Glatter anaeleza kuwa vyuo vyote 12 vya elimu ya juu Gaza vimeharibiwa au kuangamizwa, na kusimamisha kabisa mafunzo ya udaktari, uuguzi na taaluma nyingine za afya.

Hata kama miundombinu ingerudishwa leo, ingewachukua angalau miaka 10 kuandaa kizazi kipya cha wataalamu wa afya—hali inayotabiri uhaba wa muda mrefu wa wahudumu wa afya Gaza.

## wito wa hatua za haraka za kimataifa

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya wa kimataifa, suluhisho la mgogoro huu halipaswi kuishia kwenye chakula na maji pekee. Makala ya Forbes inapendekeza kupelekwa kwa hospitali za muda, meli za hospitali, vifaa vya kisasa vya uchunguzi, pamoja na programu za kimataifa za mafunzo ya wahudumu wa afya wa Kipalestina, kwa kushirikisha mataifa ya Kiarabu, Ulaya na dunia kwa ujumla.

Mgogoro wa afya Gaza ni janga la kizazi kizima. Kama ilivyoshuhudiwa wakati wa janga la UVIKO-19, ushirikiano wa kimataifa unawezekana na unaweza kuokoa maisha.

Katika hili, nchi za Kiislamu na Waislamu kwa ujumla tuna jukumu la kipekee katika kuwasaidia ndugu zao. Bila hatua za haraka na endelevu, Gaza itaendelea kubeba mzigo wa kiafya, kijamii na kiuchumi kwa miongo mingi ijayo.


Radio
Imaan FM
Arusha 90.8fm
Mwanza 106.5fm
Mbeya 90.3fm
Tabora 101.6fm
Ruvuma 94.2fm
Mtwara 90.9fm
Kigoma 92.5fm
Sikiliza
104.5FM
Dar es Salaam
Elimu Bila Mipaka




## MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

# Vijana wahamasishwe kujipamba na Uislamu

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Hatoingia Peponi mwenye chembe ya kiburi moyoni mwake." Mtu mmoja akauliza: "Hakika mtu hupenda nguo yake iwe nzuri na viatu vyake viwe vizuri." Mtume akasema: "Hakika Allah ni Mzuri na anapenda uzuri. Kiburi ni kukataa haki na kuwadharau watu." ***[Muslim].***

## Mafundisho ya tukio

Uislamu umehalalisha na kuhimiza watu kujiweka katika muonekano mzuri bila kupindukia mipaka iliyowekwa kisheria. Vilevile, Uislamu una ishara na alama zake zinazoonekana wazi kwa Muislamu, ambaye ukikutana naye ni rahisi kupata fadhila kupitia yeye kwa kumtolea salamu kutokana muonekano wake unaoashiria kuwa yeye ni Muislamu.

Mtume (rehema na amani zimshukie) alieleza mambo kumi ya fitra (maumbile), na miongoni mwa hayo ni kupunguza masharubu, kufuga ndevu, kupiga mswaki, kukata kucha, na kuondoa nywele za kwapa na za sehemu za siri. Yote haya yanahusiana na usafi wa mwonekano.

Aidha, miongoni mwa sharia zinazoonesha uhusiano wa dhahiri ya mtu na ndani yake ni hijab ya mwanamke Muislamu. Allah ameamuru wanawake wajisitiri na amewakataza kuonesha mapambo yao, huku akibainisha sababu ya kuwaamrisha kuwa ni usafi wa nyoyo za wanaume na wanawake: "Na mnapowaomba (wanawake) kitu, waombeni nyuma ya pazia, hilo ni takaso zaidi kwa nyoyo zenu na nyoyo zao." [Qur'an, 33:53].

Kwa minajili hiyo, utaona kuwa hijab ni sitara ya kisheria kwa mwanamke, vilevile ni pambo linaloonesha Uislamu wake kwa dhahiri.

## Hali ya watu wengi hivi sasa

Ni jambo la kusikitisha kuona baadhi ya Waislamu wanahisi aibu au uzito kujiweka katika muonekanao wa Kiislamu. Hali hii huashiria kasoro kubwa katika nyoyo za watu hawa.

Hakika ampendae Allah na kuridhia amri zake hufurahia kuzitekeleza kwa haraka na kwa fahari kubwa, kama walivyofanya wanawake wa Answari wakati ilipoteremka amri ya hijab. Bila kusita, haraka sana wanawake wale walichana mashuka yao na kujisitiri.

## Kujitofautisha na makafiri

Uislamu, pia umehimiza kujitofautisha na wasiyokuwa Waislamu katika muonekano wa nje, mfano kwenye suala la kupaka rangi nywele au ndevu zenye mvi. Uislamu unaruhusu kuzibadili nywele au ndevu zenye mvi kwa kuzipaka rangi iliyo na mchanganyiko wa nyeusi na nyekundu, hina, au kwa shakili ya manjano.

Hizi ni katika alama za Uislamu ambazo Masahaba na wengineo katika wema waliopita walizidhihirisha katika vitendo vyao vya wazi. Kuzibadili nywele au ndevu zenye mvi kwa kuzipaka rangi ni katika mambo ambayo watu wa Kitabu (Mayahudi na Manasara) wanajizuilia wakidhani kuwa kujipamba huko ni kinyume na uchamungu, kama wafanyavyo watawa wao.

Waislamu wa Ahlus Sunnat Wal–jama'a wanaamini kuwa imani ni kusadikisha kwa moyo, kauli ya ulimi na matendo ya viungo. Muonekano wa nje ni dalili ya yaliyomo ndani ya kiwiliwili. Ikiwa ndani kuna kheri, basi kheri hiyo lazima ionekane kwa nje; na ikiwa ni kinyume athari zake pia huonekana.

## Muonekano wa nje hautoshi

Watu wengi wanaegemea katika utekelezaji wa mambo ya wajibu wakidhani kuwa yanatosha, na wakati mwingine hujitetea kuwa muonekano wa nje si lolote kwa sababu hata wanafiki walionekana wakisali lakini walikuwa ni waongo.

Ni kweli kuwa hali ya wanafiki wakati wa Mtume (rehema na amani zimshukie) ni mfano wa wazi. Wao walihudhuria ibada ya sala msikitini kwa ria na unafiki, lakini sala haikuwazidishia kitu isipokuwa upotovu. Qur'an waliyoisikia haikuwazidishia chochoche ila upofu.

Allah anasema, nyoyo zao zilikuwa na maradhi, na kwa sababu hiyo vitendo vyao vilifichua maradhi hayo. Haikuwezekana kwao kuficha kabisa yaliyo nyoyoni mwao kwa sababu ni lazima yadhihirike. Muislamu anatakiwa aupende na kuudhihirisha Uislamu katika kila kipengele cha maisha yake ikiwa ni pamoja na muonekano wake.

Sharia ya Kiislamu imekuja kuwatofautisha Waislamu na watu wengine katika muonekano wao, mavazi yao na desturi zao. Anayetafakari mienendo ya baadhi ya vijana wetu wa leo ataona jambo hatari, nalo ni kupoteza muonekano wa Kiislamu kwenye maisha yao, hasa katika kunyoa ndevu na kupunguza masharubu.

Jambo hili linapingana na mwongozo wa Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie). Mtume ametuambia: "Kuweni kinyume na washirikina; fugeni ndevu kwa wingi na punguzeni masharubu." [Bukhari na Muslim]. Sheria ya Uislamu inakataza wanaume kujipamba kwa mitindo isiyofaa ya ndevu na nywele, kusuka nywele au kufuga/ kusokota rasta, kuvaa hereni na bangili, na kuvaa mavazi yenye chapa maarufu (brand) zinazowaunga mkono makafiri.

Aidha, sheria inakataza wanawake kutumia vipodozi vyenye kemikali na kuvaa hadharani mavazi laini yenye kuonesha maungo ya mwili. Yote haya ni mambo mabaya yaliyokatazwa katika dini. Katika hadith iliyonukuliwa na Bukahri, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Allah amewalaani wanaume wanaojifananisha na wanawake, na wanawake wanaojifananisha na wanaume."

Inasikitisha kuona vijana wengi wa zama hizi wanaiga tabia na mienendo ya wanasoka, wanamuziki na wacheza filamu wa Kimagharibi, huku wakipuuza kabisa tabia za Kiislamu alizofundisha Mtume (rehema na amani zimshukie). Vijana wengi leo hii wameacha desturi nzuri za wazazi wao ambazo wamezirithi kutoka kwa babu zao, zilizopambwa na adabu za Kiislamu na kukubaliwa na wanazuoni na kufanyiwa kazi.

Kulinda desturi njema na mila nzuri za Kiislamu ni katika maslahi makubwa yaliyothibitishwa na Uislamu, kwa kuwa zinawatofautisha na watu wengine. Kwa kupoteza desturi njema na mila nzuri za Kiislamu, haiba na utu wa Muislamu huyeyuka katika mawimbi ya utandawazi.

IDARA YA DAAWA

## Mtume ﷺ amesema:

"Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake, na Muhajir (mhamaji wa kweli) ni yule anayeacha kile alichokataza Mwenyezi Mungu."

Bukhari

رَجَب

**MAKALA**
**MALEZI**

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Mbinu za kulingania marafiki, ndugu wasio Waislamu



**Da'wah ni jukumu la kila Muislamu, lakini pia ni jukumu linalohitaji hekima kubwa, subira na ufahamu wa kina wa maumbile ya binadamu.**
**Mara nyingi changamoto kubwa hujitokeza pale tunapohisi hamu ya kuwaona marafiki au ndugu zetu wa karibu wasiokuwa Waislamu wakiuona uzuri wa Uislamu.**
**Hata hivyo, ni muhimu kuelewa ukweli wa msingi: hatuna uwezo wa kumlazimisha yeyote kuukubali Uislamu, hata kama ni mtu tunayempenda sana.**
**Allah (Subhaanahu Wata'ala) anatukumbusha wazi:**
**"Hakika wewe humuongozi umpendaye, lakini Allah humuongoza amtakaye." [Qur'an, 28:56]. Hili linatufundisha kuwa jukumu letu ni kufikisha ujumbe, si kuongoza nyoyo. Uongofu ni wa Allah pekee, na hutolewa kwa hekima Yake na kwa wakati Anaoujua Yeye.**

## Anza na kuimarisha Uislamu wako mwenyewe

Da'wah bora huanza na nafsi. Kabla ya kuwalingania wengine, ni lazima tujiimarishe sisi wenyewe katika imani, ibada na tabia. Swala zetu ziwe sahihi na zenye khushuu, tuzidishe dua, na pale inapowezekana tuswali Tahajjud tukimuomba Allah awaongoze sisi na wale tunaowapenda.

Mtu anayemuona Muislamu aliye na utulivu wa moyo, maadili mema na mabadiliko chanya katika maisha yake huanza kujiuliza: ni nini chanzo cha hali hii na kisha huanza kuvutiwa na Uislamu pale anapojua ndio dira ya yule anayemtamani.

## Onyesha Uislamu kwa vitendo, si kwa mabishano

Uislamu hauenezwi kwa hoja kali au mijadala ya kushindana. Mara nyingi, mabishano huwafanya watu wajifunge zaidi. Badala yake, mwenendo mwema ndio da'wah yenye nguvu zaidi. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliwalingania watu kwa tabia yake: alikuwa mkweli, mvumilivu, mwenye kusamehe na mwenye huruma hata kwa waliomuumiza.

Marafiki zako wanapokuona ukiwa mwaminifu, mpole, mwenye kuheshimu wengine na mwenye kusimama imara katika misingi yako, wataona tofauti. Huna haja ya kuhubiri kila mara; tabia yako itazungumza yenyewe.

## Heshimu uhuru wao wa kuchagua

Allah anasema: "Hakuna kulazimisha katika dini." [Qur'an, 2:256].

Hili ni somo muhimu sana katika da'wah. Usimfanye rafiki yako ahisi anasukumwa au kushinikizwa. Ikiwa atauliza maswali kuhusu Uislamu, jibu kwa unyenyekevu na uaminifu. Kama hujui jibu, sema hujui na utafute baadaye. Hilo hujenga heshima na kuaminika.

Kama ataonyesha kutopenda kuzungumzia dini, heshimu hilo. Da'wah si lazima iwe kwa maneno; subira na dua vina nafasi kubwa.

## Chagua muda na namna sahihi

Si kila wakati ni mzuri kwa da'wah. Hekima ni kujua wakati sahihi wa kuongea na muda wa kunyamazea. Mazungumzo yakija kwa kawaida—kwa mfano mtu akiuliza kwa nini hunywi pombe au kwa nini unavaa kwa namna fulani—hapo ndipo fursa nzuri ya kuelezea kwa upole, bila mashambulizi au lawama.

Zungumza kwa lugha rahisi, epuka misamiati migumu au istilahi za Kiarabu zisizoeleweka. Lengo si kumchanganya, bali kumfanya aelewe.

## Omba dua na umwachie Allah matokeo

Jambo kubwa na lenye nguvu zaidi katika da'wah ni dua. Mwombe Allah afungue nyoyo, akupe hekima na akulinde na kukata tamaa. Hakuna roho ya nzuri itakayopotea bila uongofu kwa idhini ya Allah. Watu tunaodhani wako mbali kabisa na Uislamu wanaweza kuja kuukubali kwa mapenzi ya Allah, hata baada ya muda mrefu. Fanya unaloweza kwa uwezo wako, kwa upole na kwa mapenzi, kisha muachie Allah yaliyobaki. Hata kama hutashuhudia matunda ya jitihada zako, huenda siku moja wakakumbuka kuwa waliwahi kukutana na Muislamu mwenye tabia njema sana, na hilo likawa mwanzo wa safari yao ya uongofu.

Na Allah Anajua zaidi.






UKHTI FATIMA SS

# Kwa nini watu tunacheka? mtizamo wa saikolojia

**Kicheko ni moja ya tabia za kibinadamu zinazopatikana karibu katika tamaduni zote duniani.**

**Watoto huanza kucheka wakiwa wachanga, watu wazima hucheka wanapokuwa na marafiki, na hata katika nyakati ngumu, kicheko bado hujitokeza. Lakini swali la msingi la kisaikolojia ni hili: kwa nini watu tunacheka?**

**Je, ni mzaha tu unaotusukuma kucheka, au kuna sababu za kina zaidi katika akili na hisia zetu?**

**Kwa muda mrefu, wanasaikolojia, wanafalsafa na watafiti wa ubongo wamejaribu kuelewa asili ya kicheko.**

**Ingawa hakuna nadharia moja inayoweza kueleza kila aina ya ucheshi, kuna maelezo kadhaa muhimu ambayo yanatusaidia kuelewa kwa nini kicheko ni sehemu ya maisha ya binadamu.**

## Kicheko, matokeo ya mshangao

Moja ya nadharia maarufu ni nadharia ya kutolingana (incongruity theory). Kwa mujibu wa mtazamo huu, watu hucheka pale kitu kinapotokea kinyume na matarajio yao. Akili ya binadamu hupenda mifumo na mpangilio. Inapokutana na jambo lisilotarajiwa lakini lisilo na madhara, hutafsiri hali hiyo kama ya kuchekesha. Ndiyo maana mzaha wenye mistari (punchline) isiyotegemewa mara nyingi hutufanya tucheke.

Hata hivyo, si kila mshangao huleta kicheko. Tukio la kushtua au lenye maumivu halitachekesha. Hapa ndipo wanasaikolojia walipoendelea zaidi kuelewa mpaka kati ya kichekesho na tukio la kuumiza.

## Nadharia ya "ukiukaji usio na madhara"

Nadharia ya kisasa zaidi inayokubalika sana inajulikana kama 'benign violation theory'. Kwa mujibu wa nadharia hii, kitu huwa cha kuchekesha pale kinapokiuka kanuni fulani za kijamii, kimaadili au kimantiki, lakini ukiukaji huo hauonekani kuwa hatari au wa kuudhi.

Mfano ni mzaha unaovunja taratibu za kawaida za mazungumzo, au tukio la kimwili lisilo la kuumiza kama mtu kuteleza bila kuumia.

Ikiwa ukiukaji huo unaonekana kuwa mkubwa, wa kuogofya au wa kuumiza, basi kicheko hutoweka. Hii inaeleza kwa nini watu tofauti hucheka vitu tofauti; kinachoonekana kuwa "si tatizo" kwa mtu mmoja, kinaweza kuwa cha kuudhi kwa mwingine.

## Kicheko kama njia ya kuachilia msongo wa mawazo

Wanasaikolojia wengine wanaeleza kicheko kupitia nadharia ya ponyo ya kihisia (relief theory). Kwa mtazamo huu, kicheko ni njia ya kuachilia mkazo wa kihisia au "nishati ya neva" iliyokusanyika.

Wataalamu wanasema nadharia hii inaleeza kwa watu hucheka sana katika mazingira yenye msongo kama kabla ya mtihani, wakati wa mazishi (kwa kicheko cha neva), au baada ya hali ya hofu kupita.

Kicheko husaidia mwili kupunguza homoni za msongo wa mawazo, na kuleta hisia ya nafuu. Kisaikolojia, ni kama njia, tundu. (valve) kupitia hiyo shinikizo la ndani linayopungua.

## Kicheko na hisia za ubora

Nadharia ya zamani zaidi, inayotokana na falsafa za kale, ni nadharia ya ubora (superiority theory). Kwa mujibu wa mtazamo huu, watu hucheka wanapojihisi bora kuliko wengine, hasa wanapoona makosa, udhaifu au bahati mbaya ya mtu mwingine.

Ingawa nadharia hii haielezi kila aina ya kicheko, bado inaonekana katika baadhi ya vichekesho vya kejeli au mzaha unaomhusisha "mhanga" wa ucheshi.

## Kicheko kama gundi ya kijamii

Kisaikolojia na kimaumbile, kicheko kina jukumu kubwa la kijamii. Tafiti zinaonyesha kuwa watu hucheka mara nyingi zaidi wakiwa na wengine kuliko wakiwa peke yao. Kicheko huimarisha uhusiano, hujenga hali ya kuaminiana, na huashiria usalama wa kijamii. Ndiyo maana vicheko vya pamoja huleta hisia ya ukaribu na mshikamano.

Kwa mtazamo wa mageuzi ya binadamu, kicheko kinaweza kuwa kilitumika kama ishara ya "hali salama" katika makundi ya kale ya wanadamu, kikionyesha kuwa hakuna tishio la haraka.

Kwa jumla, watu tunacheka kwa sababu nyingi: mshangao usio na madhara, uachiliaji wa msongo wa mawazo, hisia za kijamii, na hata utambuzi wa makosa ya kimantiki.

Kicheko si burudani tu; ni chombo cha kisaikolojia chenye nguvu kinachosaidia afya ya akili, huimarisha mahusiano, na hutuwezesha kukabiliana na changamoto za maisha kwa mtazamo mwepesi zaidi. Huenda hatutaweza kamwe kufafanua kicheko kwa nadharia moja kamili, lakini labda hilo ndilo uzuri wake—kicheko kinabaki kuwa siri yenye furaha katika maisha ya mwanadamu.

NA UKHTI FATIMA



# Kanuni 8 za Kiislamu kuelekea ustawi wa kifedha

**Tunaishi katika dunia inayosukumwa na matumizi makubwa, mashindano ya mali na kasi ya maisha. Katika mazingira haya, ni rahisi kwa Muislamu kupoteza mwelekeo na kuanza kuyaona mafanikio ya kifedha kama lengo kuu la maisha.**
**Hata hivyo, Uislamu unatupa mwongozo kamili unaotuwezesha kusawazisha kati ya ustawi wa kifedha na ukuaji wa kiroho. Uislamu haukatazi utajiri, bali unaweka kanuni na misingi ya kuutumia kwa njia yenye baraka, hekima na manufaa duniani na akhera.**

## Mosi, mali kwa mtazamo wa Kiislamu

Katika Uislamu, mali hujulikana kama rizq—kipato na neema inayotoka kwa Allah (Subhaanahu Wata'ala). Qur'an inatuambia wazi kuwa binadamu wameumbwa na mapenzi makubwa ya mali. Hata hivyo, mali si tu chombo cha matumizi, bali pia ni mtihani. Inaweza kumleta mtu karibu na Allah au ikampeleka mbali Naye, kutegemea namna anavyoitazama na kuitumia.

Muislamu anatakiwa kuelewa kuwa mali anayoipata si kwa uwezo wake binafsi pekee, bali kwa mapenzi ya Allah. Mtazamo huu humjenga mtu kuwa mnyenyekevu, mwenye shukrani na anayejua kuwa mali yote ni amana. Kuweka mkazo mkubwa katika mali ya dunia pekee huleta hofu na wasiwasi wa kifedha, lakini kufanya kazi kwa ajili ya Akhera huleta utulivu wa moyo na ridhaa.

## Weka malengo yenye mwelekeo wa dini

Uislamu unahimiza mipango na nidhamu. Muislamu anatakiwa kuwa na malengo ya kifedha yaliyo wazi na yenye mwelekeo sahihi, yakijumuisha mahitaji ya kidini kama Hajj na Umrah, majukumu ya kifamilia, elimu ya watoto na maandalizi ya uzeeni.

Malengo yasiyo wazi humfanya mtu kutumia mali bila mpangilio na kuishi maisha ya presha ya kifedha.

Malengo ya kifedha yanapowekwa kwa nia njema na kwa kuzingatia ridhaa ya Allah, humsaidia Muislamu kutumia mali kama chombo cha ibada, si kama lengo lenyewe.

## Tafuta kipato na tumia kwa halali

Uislamu unaweka msisitizo mkubwa katika uhalali wa kipato. Muislamu anatakiwa ajiepushe na vyanzo vya kipato vilivyoharamishwa kama riba, kamari, udanganyifu na biashara haramu.

Kipato halali, hata kama ni kidogo, huleta amani ya moyo na baraka katika maisha,.

Vilevile, matumizi yanapaswa kuwa ya wastani. Uislamu hauhimizi ubakhili wala ubadhirifu. Kutumia kwa familia, kusaidia wahitaji na kuchangia jamii, kwa nia njema, huhesabika kuwa ni sadaka. Matumizi yenye maadili huimarisha uhusiano wa kifamilia, kijamii na huondoa migogoro ya kifedha isiyo ya lazima.

## Jenga nidhamu ya bajeti na ishi ndani ya uwezo

Moja ya misingi ya ustawi wa kifedha ni nidhamu ya matumizi. Uislamu unahimiza kuishi ndani ya uwezo, kupanga mapato na matumizi, na kuepuka maisha ya mikopo na madeni yasiyo ya lazima.

Bajeti humsaidia Muislamu kujua mipaka yake, kulinda heshima ya mali na kuepuka mzigo wa kifedha unaoweza kumlemea kisaikolojia na kiroho.

## Toa zaka, sadaka

Zaka ni nguzo muhimu ya mfumo wa kiuchumi wa Kiislamu. Ni wajibu kwa mwenye uwezo, ikilenga kutakasa mali na kusawazisha jamii. Mbali na Zaka, Muislamu anahimizwa kutoa sadaka za hiari (sadaqah), ambazo huongeza baraka na kuimarisha mshikamano wa kijamii.

Sadaka humlinda mtu dhidi ya magonjwa ya moyo kama kiburi, tamaa na mapenzi ya dunia kupita kiasi, na humjengea moyo wa huruma na shukrani.

## Wekeza katika njia halali

Kuacha mali bila kuifanyia kazi huifanya ipungue thamani kutokana na mfumuko wa bei na wajibu wa Zaka. Uislamu unahimiza uwekezaji halali unaozingatia misingi ya Sharia, kama biashara halali, miradi ya kijamii na mali zisizohusisha riba.

Kwa mtazamo wa Kiislamu, uwekezaji si kwa ajili ya dunia pekee, bali ni njia ya kukuza uwezo wa kusaidia familia, jamii na kuongeza sadaka—hatimaye kuwekeza kwa ajili ya Akhera.

## Dhana ya baraka katika mali

Kiini cha uchumi wa Kiislamu ni baraka. Baraka huifanya mali iwe na manufaa makubwa hata kama ni ndogo. Mtu anaweza kuwa na kipato kidogo lakini akaishi kwa utulivu, akatosheka na akaweza kuwasaidia wengine.

Baraka hupatikana kwa uhalali wa kipato, nia njema, matumizi sahihi na kutotumia mali kinyume na maadili ya Uislamu.

## Jilinganishe na walio chini yako

Uislamu unatuonya dhidi ya mtazamo wa uhaba unaosababisha uchoyo, hofu ya kifedha na kutoridhika. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alitufundisha tuwaangalie walio chini yetu kimaisha ili tujifunze kushukuru, badala ya kuwatazama walio juu na kutamani mali yao.

Allah humpa kila mmoja kwa hekima Yake, na mali ya mtu mwingine ni mtihani wake binafsi.